**Kesi** ya Ole Sabaya sasa kunguruma siku 14 mfululizo

UKURASA 2



**Washikiliwa** kwa tuhuma za kumuua dereva bodaboda

UKURASA 2




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580644

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII


www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


RIPOTI MAALUM

# Shule yawakataa watoto wagonjwa

• **NI** wenye matatizo ya moyo, pumu, vidonda vya tumbo, uongozi wakiri, serikali yatoa neno... *Endelea ukurasa 4*



## Samia, Rais wa Burundi wakubaliana mambo manne

UKURASA 2

Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye, katika Ikulu ya Ntare House, jijini Bujumbura jana, akiwa katika ziara ya kitaifa ya siku mbili nchini humo. **PICHA: IKULU**

# Mawakala waanika makali tozo za miamala ya simu




UKURASA 3

**MICHEZO** **UCHAGUZI MKUU TFF PALE PALE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia, Rais Burundi wakubaliana manne

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan na mwenzake wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, wamekubaliana mambo manne ikiwamo kuondoa vikwazo vya kibiashara na kujenga miundombinu ya barabara na reli ili kuunganisha biashara mipakani.

Viongozi hao wamekubaliana kushirikiana kujenga barabara zinazounganisha nchi mbili, ikiwamo ya Kasulu/Nyakanazi/Manyovu/Rumonge/Itaza na kuharakisha ujenzi wa kituo cha pamoja mipakani, Manyovu na Mugina.

Makubaliano mengine waliyowekeana saini ni mkataba wa ufundishaji lugha ya Kiswahili na Kifaransa kwenye nchi hizo mbili.

Rais Samia aliyasema hayo jana akiwa Burundi katika ziara ya kikazi wakati marais hao walipozungumza na waandishi wa habari.

Rais Samia alisema ziara yake imelenga masuala makubwa manne ikiwamo kutoa shukrani kwa ushiriki wa Burundi katika msiba wa Hayati Dk. John Magufuli na kuwapongeza kwa sherehe za kumbukumbu ya uhuru wao na kuendeleza uhusiano wa nchi mbili.

Alisema kwenye mazungumzo yao kabla ya mkutano huo na wanahabari, yalijikita katika uchumi, kukuza biashara na uwekezaji, akibainisha kuwa biashara imeongezeka kwa nchi mbili kutoka Sh. bilioni 83.9 mwaka 2015 hadi Sh. 200.1 mwaka 2019.

Rais alisema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 18 kutoka Burundi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 209.4 na kutoa ajira 3,544 kwa Watanzania ukiwamo mradi mkubwa wa kiwanda cha mbolea Itracom chenye thamani ya Dola milioni 180. Rais Samia alisema Tanzania imewekeza kampuni mbalimbali Burundi, ikiwamo Azam, Azania, Interpetro Ltd na Benki ya CRDB na kwamba kiwango cha uwekezaji hakijatumika ipasavyo kulinganishwa na fursa zilizopo.

Rais Samia aliwakaribisha wafanyabiashara wa Burundi kuja kuwekeza Tanzania kwenye sekta za viwanda, madini, kilimo na utalii kutokana na fursa zilizopo nchini.

Alisema ili kukuza biashara hiyo wamejadiliana na mwenzake kuboresha miundombinu ya usafiri na kukuza uchukuzi, ikiimarika itaboresha biashara na kukuza uchumi baina ya nchi hizo.

"Niendelee kuwaomba wafanyabiashara wa Burundi kuendelea kuitumia Bandari ya Dar es Salaam kuendelea kupitisha mizigo, ninafahamu kwa asilimia 95 ya mizigo ya Burundi inapitishwa Tanzania. "Mwaka jana mlipitisha tani 476,809 za mizigo, tutaendelea kuboresha miundombinu ili iwe ya ufanisi," alisema.

Kuhusu usafiri wa anga, Rais Samia alisema Machi mwaka huu, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) lilisitisha safari zake Burundi kutokana na Covid-19 na kwamba maandalizi ya kurejesha yanaendelea.

"Nishati ya umeme ni kivutio cha kukuza uchumi na uwekezaji, Rais Ndayishimiye amenihakikishia vituo vitatu vinaendelea kujengwa na wa kwetu wa Bwawa la Nyerere ukikamilika utazalisha megawati 2,115, pia tutauza," alisema.

Rais Samia alisema mazungumzo yao hayakuweka mbali uhusiano wa kukuza teknolojia ya mawasiliano na kwamba mkongo wa mawasiliano wa taifa umefika Burundi na nchi hiyo inaruhusu nchi hiyo kupitia taasisi za mawasiliano nchi mbili kutumia mkongo huo.

Rais Ndayishimiye alisema Tanzania pamoja na Burundi kwa vipindi tofauti, zilipata pigo kwa kuwapoteza marais wao, Hayati Dk. Magufuli na Piere Nkurunziza na wamesikitishwa na tukio la hivi karibuni la kuungua kwa Soko la Kariakoo ambalo hutumiwa na nchi yake na Afrika Mashariki kwa ujumla.

Alisema anaishukuru Tanzania kwa uzalendo wake na ushirikiano hata katika kipindi cha Covid-19 na wamekubaliana kuongeza ulinzi na usalama mipakani, kukabili ugaidi, silaha haramu na biashara haramu ya binadamu.

"Katika kilimo, mifugo Burundi tutashirikiana na Tanzania, tayari Itracom, kiwanda cha mbolea kitakajengwa Tanzania, tunakaribisha wananchi wa nchi mbili kuwekeza zaidi. "Tuendelee kukabiliana na corona kwenye mipaka yetu, ni imani yetu tutaendelea kushirikiana kwa manufaa ya nchi zetu," alisema Rais Ndayishimiye.



Askari wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Magereza, wakiimarisha ulinzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha jana, wakati kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake ikisikilizwa. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Kesi ya Sabaya kunguruma kwa siku 14 mfululizo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya jinai namba 66 ya mwaka 2021 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, na wenzake, umeondoa mashtaka mawili ya unyang'anyi wa kutumia silaha na kufungua mashtaka mengine mapya matatu.

Kesi hiyo ilitajwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, washtakiwa hao walikamatwa tena na kufunguliwa mashtaka mengine matatu katika kesi ya jinai namba 105 ya mwaka 2021.

Baada ya kukamatwa, walisomewa mashtaka hayo mapya na maelezo ya awali na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Tumaini Kweka, alidai mahakamani huko kwamba shauri namba 66 lilikwenda kwa ajili ya kusikilizwa kwa mashahidi kutoa ushahidi wao, lakini waliomba kuliondoa shauri hilo mahakamani.

"Mheshimiwa Hakimu, tunaomba kuliondoa shauri hili chini ya kifungu namba 91(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa maboresho mwaka 2019," alidai na kuiomba mahakama kuwafungulia washtakiwa hao mashtaka mengine mapya.

Wakili Chavula, akisoma mashtaka mpaya, alidai shtaka la kwanza ni la unyang'anyi wa kutumia silaha linalowakabili washtakiwa hao.

Chavula alidai mshtakiwa wa kwanza Ole Sabaya (34), Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. milioni 2.769, mali ya Mohamed Saad na baada ya wizi huo walitumia silaha ya bunduki kuwatisha waliokuwa kwenye duka hilo.

Shtaka la pili, ni unyang'anyi wa kutumia silaha, ikidaiwa washtakiwa hao kwa pamoja wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha kiasi cha Sh. 390,000, mali ya Bakari Msangi na baada ya wizi huo walimfunga kwa pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Katika shtaka la tatu ambalo ni la wizi wa kutumia silaha, ilidaiwa mahakamani huko kuwa Ole Sabaya na wenzake, Februari 9 mwaka huu, Mtaa wa Bondeni jijiji Arusha, waliiba simu moja aina ya Tekno na fedha kiasi cha Sh. 35,000, mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika makofi, ngumi, mateke na walitumia silaha kumtisha ili wapatiwe fedha na mali walizoiba.

Baada ya kusome maelezo ya mashtaka hayo, washtakiwa wote walikana mashtaka hayo.

Katika hatua nyingine, Hakimu Mkazi Mwandamizi Odira Amworo, alisema kesi hiyo itasikilizwa kwa siku 14 na hadi kufikia Julai 30, mwaka huu, inatakiwa iwe imemalizika.

"Nimekuja kwa kazi maalumu ya kusikiliza kesi hii na ndiyo imenileta hapa, na itasikilizwa kila siku hadi kufikia Julai, mwaka huu, ninatakiwa niwe nimeshamaliza kesi ambayo imenileta huku," alisema hakimu huyo kisha akiahirisha hadi Julai 19, mwaka huu, itakapotajwa tena na washtakiwa kurudishwa rumande katika Gereza la Kisongo.

# Watuhumiwa kumuua dereva wa bodaboda

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linawashikilia watuhumiwa wa uhalifu 46 kati yao, wanne akiwamo mwanamke wanatuhumiwa kumuua dereva wa pikipiki Jumanne Mussa (30) mkazi wa eneo la Tungwi Songani, Kigamboni, Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa hao wanne wanadaiwa Julai 3, mwaka huu, walikula njama kwa kumtumia mwanamke huyo aliyefahamika kwa jina la Malkia Luhende (42) kutekeleza mauaji hayo. "Uchunguzi wetu umewezesha kupatikana kwa wahalifu hawa (bila kuyataja majina ya watatu) wakiwa na baadhi ya vielelezo muhimu, uchunguzi unaendelea," alisema. Pia alisema wamewakamata watu wawili wanaojihusisha na vitendo vya utapeli ambao ni Oswald Fidolini (47) maarufu kwa jina la Mbilo na Melkizedeck Mathayo (49) maarufu kama Hungo.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakijipatia fedha kutoka kwa wananchi kwa njia ya vitisho kwa kuwatishia na kutengeneza mazingira ya kuichafua serikali.

"Mara kadhaa wamekuwa wakijiita maofisa wa usalama wa taifa na makamisha wa polisi na maofisa wa TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa). Watu hawa si watumishi wa serikali, tumewakamata," alisema.

Kamanda Muliro alisema wamewapata watuhumiwa wengine zaidi ya 40 ambao wamekuwa wakijihusisha na unyang'anyi wa kutumia nguvu, kuvunja nyumba na kuiba, kupora kwa kutumia pikipiki maarufu kama vishandu.

Alisema katika matukio hayo wamekamata pikipiki tatu zinazotumiwa na wahalifu hao, runinga nane na kompyuta mpakato.

Kamanda huyo aliwaomba wananchi waendelee kutoa taarifa ili Dar es Salaam iendelee kuwa salama.

HABARI KITAIFA

# Awahakikishia mazingira safi ya uwekezaji

**Na Enock Charles**

SERIKALI imewahakikishia wawekezaji mazingira mazuri na sera zinazotabirika nchini.

Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Exaud Kigahe, alisema hayo juzi alipozungumzia mipango ya serikali kwa wawekezaji wa ndani na nje, alipozindua kinywaji kipya chenye chapa ya Kiwingu kutoka Kampuni ya Kilimanjaro Biochem Limited (KBL) jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali inajitahidi kuweka mazingira rafiki ili kuwasaidia wawekezaji nchini kama ilivyoahidi.

"Tukiwa na kampuni kama hizi au 100, maana yake, yanaweza kuiwezesha serikali kuendesha mipango yake kirahisi kwa kuwa na uhakika wa mapato yatokanayo na Sekta ya Viwanda," alisema.

Alisema serikali imeanza kuangalia tena sheria ambazo ni kikwazo kwa wawekezaji kama ilivyoagizwa na Rais Samia Suluhu ambaye ameweka wazi kuwa madereva wa utawala wa sita wa uchumi ni watu kutoka sekta binafsi.

Alisema wizara inafanya kazi katika kuimarisha na kuanzisha mbinu mpya za kirafiki ili kuwezesha sekta binafsi kushiriki katika uchumi kwa uwezo wake wote.

Kiwanda cha KBL ambacho kiko katika Kijiji cha Kifaru wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, kimewekeza Sh. bilioni 11.5 katika uzalishaji wa kinywaji aina ya Kiwingu, kikizalisha takribani lita 20,000 kwa siku. Mwenyekiti wa KBL, Mehul Patel, alisema kampuni yake hatimaye imeanzisha bidhaa hiyo kwenye soko baada ya utafiti uliofanyika kwa zaidi ya miezi 10 juu ya kile watumiaji wanakosa kutoka katika bidhaa nyingi za pombe nchini.

"Wateja wanatarajia ladha ya kipekee na ya kupendeza, harufu ya kupendeza, hisia ya hangover ya elastic na bei rahisi.

"Kabla ya kuja na bidhaa hiyo, tulifanya utafiti kwa vikundi tofauti vya umri na kuhitimisha kuwa hakuna kinywaji kinachokidhi vigezo hivi kila wakati," Patel alisema.

Alisema kuwa uwekezaji wao mpya utaongeza mapato ya sasa ya Sh. bilioni 24 hadi kufikia bilioni 50 katika miaka mitatu ijayo.



Ujenzi wa daraja jipya la vyuma la Mto Suguti linalounganisha vijiji vya Wanyere na Kataryo, wilayani Musoma, mkoani Mara, ukiwa umekamilika na kufanya wakazi wa maeneo hayo, kuachana na matumizi ya daraja la miti (kushoto), ambalo lilikuwa ni hatari hasa nyakati za mvua. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mawakala waanika makali tozo za miamala ya simu

**Na Romana Mallya**

MAWAKALA wanaotoa huduma za kifedha wamelia na ongezeko katika tozo za miamala ya simu, huku wakibainisha kupungua kwa wateja wanaotaka kupatiwa huduma kwa madai kwamba makato ni makubwa.

Wakizungumza na Nipashe jana mkoani Dar es Salaam kwa nyakati tofauti baada ya tozo hizo kuanza kutumika juzi, mawakala hao walisema wateja wanapofika kwenye ofisi zao baada ya kuulizia makato ya fedha wanazotaka kutoa, wanaondoka bila kupata huduma.

Grace Ng'wandu, walaka anayetoa huduma hiyo eneo la Mwenge, alisema kwa hali inavyoendelea, mawakala wengi wanataka kuachana na biashara hiyo kutokana na kukosa wateja.

"Niko kwenye makundi ya mawakala na hali inavyoendelea ni kwamba biashara tutazifunga. Kuna wengine wanasema tangu asubuhi wamehudumia mteja mmoja (wakati huo ikiwa ni saa 10:16 jioni jana) kwa sababu makato ni makubwa. Wateja wanasema ni bora wapeleke fedha wenyewe kwa watu wanaotaka kuwatumia kuliko makato hayo," alisema.

Ng'wandu alisema biashara kwa sasa imekuwa ngumu kwa sababu kabla ya makato, alikuwa akihudumia kwa siku wateja hadi 120, lakini kwa sasa wanaweza wasifike 10.

"Hapa nimetoka kulipa kodi ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) na nimelipa ya manispaa. Kiukweli wanatakiwa kupunguza hizo tozo angalau wangeongeza kwa kila muamala hata Sh. 500 afadhali na wana uwezo wa kuingiza fedha nyingi," alisema.

Wakala huyo alisema kiasi anacholipwa kutokana na kazi hiyo ni kidogo na ameweka mtaji wake kwenye biashara na ulinzi lakini bado hatari ni zake na serikali inachukua fedha nyingi.

Neema Frederick, anayefanya shughuli hiyo eneo la Msasani, alisema siku nzima juzi amepata wateja watatu tu wakati kabla ya tozo hizo kuanza, alikuwa akihudumia watu 30 hadi 40 kwa siku.

"Kabla ya tozo mtu alikuwa anatumiwa fedha Sh. 5,000 kwa ajili ya chakula ili umtolee baada ya makato alikuwa anaondoka na Sh. 4,500 lakini kwa sasa kwa tozo hizi mtu anapata Sh. 3,800. Wengi wanakuja wakijua makato ni kiasi gani kwa fedha ambazo wanataka kutoa wanaondoka bila kutaka huduma," alisema.

Wakala Angel Tenga anayefanya shughuli hiyo maeneo ya Gongo la Mboto, alisema hali ni mbaya kutokana na wateja kwa sasa wamepungua kutokana na tozo hizo.

"Kwa kweli wateja wamepungua siwezi kudanganya. Awali nilikuwa nahudumia zaidi ya wateja 10, lakini kwa sasa wakifika watano unamshukuru Mungu. Tunaomba serikali iliangalie hili ikiwezekana wapunguze," alisema.

Mfanyakazi kwenye duka la uwakala lililoko Mwenge, Khadija Rumondo, alisema kabla ya tozo hizo mpya kuanza kutumika kuanzia juzi, walikuwa wakihudumia zaidi ya wateja 100 kwa siku kuanzia juzi wateja waliowapata ni wawili tu.

"Kwa leo (jana) huduma ambazo tunatoa ni za benki, hizi zingine za mitandao ya simu kwa kweli wateja hakuna. Ombi letu kwa serikali wapunguze kidogo hizi kodi kwa sababu watu wanakwambia yaani nitoe Sh. 600,000 nikatwe 12,000 kweli?

"Mimi ni mfanyakazi hapa. Hali hii ikiendelea ina maana nitakosa kazi, mhusika ataona bora akae mwenyewe, kuliko kuajiri mtu," alisema.

KATAMBI AWAPOZA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, amewataka Watanzania wasilalamike juu ya tozo mpya za makato ya miamala za simu za mkononi kwa kuwa serikali imelenga kuwaletea maendeleo.

Katambi ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, alibainisha hayo jana kwenye mkutano wa hadhara, wakati akizungumza na wananchi wa Ibadakuli. Alisema tozo hizo mpya zimelenga kuongeza mapato ya serikali, ili kuwatekelezea wananchi miradi mbalimbali ya maendeleo.


## TANGAZO LA MNADA / NOTISI

**MALAPA AUCTION MART CO. LTD.,** KWA NIABA YA **CRDB BANK PLC.** TUNATOA NOTISI NA TANGAZO KWA WAMILIKI WA DHAMANA ZIFUATAZO WAWE WAMELIPA MADENI YAO YOTE YA CRDB BANK PAMOJA NA GHARAMA ZA DALALI. KINYUME CHA HAPO TUTAUZA MALI/ DHAMANA ZAO ILI KUFIDIA MADENI YAO.

| S/N | DHAMANA | USAJILI | MMILIKI/MDHAMINI | MAHALI ILIPO | TARERHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | DAUDI GABRIEL SANGA | MBEYA MJINI | 30 JULY 2021 NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | MATHIAS PASCAL MASANJA | MANYONI Plot No. 1632 Block "Kaloleni" | 30 JULY 2021 NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | MATHIAS PASCAL MASANJA | MANYONI Plot No. 1052 Block "AA" | 31 JULY 2021 NA KUENDELEA |
| 4 | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | MACHEMBE SALUM NDUSHI | MANYONI Plot No. 247 Block "CC" | 31 JULY 2021 NA KUENDELEA |
| 5 | NYUMBA | TITTLE 4382 LO. 97480 | DANIEL ABIHUDI MWEMBE | SUMBAWANGA Plot No. 351 Block "R" | O1 AGUST 2021 NA KUENDELEA |
| 6 | NYUMBA | TITTLE 22334 LO. 156069 | NASHON ROBERT | TABORA MJINI Plot No. 15 Block "2" | 2 AGUST 2021 NA KUENDELEA |
| 7 | NYUMBA | TITTLE 42032 LO. 142461 | MENAS MASENGO | IRINGA MJINI Plot No. 350 Block "J" | 2 AGUST 2021 NA KUENDELEA |
| 8 | NYUMBA | TITTLE 30014 LO. 198783 | NUHU DANIEL ANDREA | SHINYANGA Plot No. 868 Block "H" | 4 AGUST 2021 NA KUENDELEA |
| 9 | NYUMBA | TITTLE 4116 LO. 423348 | GEORGE PATRICE NYASWE | SHINYANGA Plot No. 590 Block "TT" | 5 AGUST 2021 NA KUENDELEA |
| 10 | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | NUHU DANIEL ANDREA | SHINYANGA Plot No. 1175 Block "GG" | 5 AGUST 2021 NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNADA UTAFANYIKA SEHEMU DHAMANA ILIPO.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA 25% YA BEI PAPO HAPO NA 75% NDANI YA SIKU 14 BAADA YA MNADA.
3. ENDAPO MTEJA ATASHINDWA KULIPA NDANI YA SIKU 14 KIASI KILICHOLIPWA AWALI HAKITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA.
4. GHARAMA ZA KUBADILI HATI MILIKI NI JUU YA MNUNUZI MWENYEWE.
5. DHAMANA ITAUZWA KAMA ILIVYO.

116361302

RIPOTI MAALUM

# Shule yakataa wanafunzi wagonjwa

## •Ni wenye magonjwa sugu, mkuu akiri 'hawana mpango nao', serikali yatoa neno

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NI ngumu kidogo kuamini mwanafunzi anayejiunga na shule lakini huduma za awali anazopatiwa zina sura zaidi kwenye afya - kliniki, lengo kuu linaelezwa ni kuthibitisha ubora wa afya ya anayejiunga na masomo, katika tafsiri inayofanana zaidi na mchujo wa usaili kwa wanaojiunga na ajira ya majukumu maalum kama jeshi.

Kimsingi, ni mzizi wa dodoso wenye sura 'jambo limezua jambo', ushuhuda wa Nipashe ukianzia kwenye foleni ya mzazi akimsubiri mwanawe kupimwa afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ili kukidhi vigezo vya shule anayokwenda kujiunga.

Mbali na maelezo ya mzazi, hata maandiko yenye maagizo ya shule yalisisitiza kuwa "mwanafunzi apimwe kweli na akifika huku atapimwa tena ikibidi".

Ni mkasa ulioipeleka Nipashe mbali kwenye marejeo ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo 'bila kupindishwa' inahimiza mwanafunzi asibaguliwe kwa namna yoyote, ikiwamo tafsiri ya kiafya.

Sheria hiyo na marejeo yake ya mwaka 2014, inapatafsiri mahali hapo wanaposoma watoto kwa lugha "...'shule iliyoidhinishwa' maana yake ni shule iliyoanzishwa chini ya sheria hii na inajumuisha eneo lolote au taasisi iliyotangazwa hivyo chini ya masharti ya sheria hii."

Kufikia majumuisho ya vitendawili hivyo, mwandishi akajielekeza moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule hiyo ya Sekondari ya Wasichana Huruma, Sister Chrispiana Ikaku, kupata ukweli na mantiki ya angalizo hilo ambalo halijazoeleka maeneo mengi.

Naye bila kusita akatoa ufafanuzi wa kinachojiri chini ya uongozi wake akitamka: "Shule hairuhusu kupokewa kwa mtoto yeyote mwenye matatizo ya kiafya."



Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI, Gerald Mweli

**KINACHOJIRI SHULENI**

Kwa kurejea, barua iliyotolewa na shule hiyo ya mkoani Dodoma kwa wanafunzi wapya wanaojiunga nayo mwaka huu (Nipashe ina nakala yake), inaelekeza kuwa haiko tayari kumpokea mwanafunzi mwenye tatizo la maradhi yanayoorodheshwa jumla yake matano.

Barua inasisitiza: "Masomo yanahitaji mwanafunzi awe na afya nzuri. Kwa hiyo, shule haipokei wanafunzi wenye matatizo yafuatayo: Moyo; kifafa; allergy (mzio), vidonda vya tumbo na pumu (asthma).

"Mtoto apimwe kweli, asijaziwe fomu tu. Mwanafunzi atapimwa tena shuleni endapo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo."

Nipashe ilipozungumza na Mkuu wa Shule hiyo iliyoko jijini Dodoma, Sister Chrispiana, ambaye sasa yuko katika mchakato wa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano, alikiri maudhui ya barua yake kwamba ndiyo maelekezo ya shule kwa wasailiwa wapya wa masomo.

Kwa mujibu wa Sister Chrispiana, msingi wa uamuzi wao huo unatokana na alichodai shule yao haina uwezo wa kuwahudumia wanafunzi wenye maradhi hayo.

"Hiyo barua mliyonayo, inaelekeza vizuri hatupokei mtoto mwenye tatizo la kiafya hapa shuleni kwetu, ni lazima mtoto apimwe kabla hajafika hapa na kama itaonekana kuna ulazima, atapimwa tena akifika hapa," alisisitiza.

**KAULI YA SERIKALI**

Hapo ndipo udadisi wa Nipashe ukahamia serikalini, ambako ndiko wasimamizi wakuu wa sheria, sera na miongozo mahususi kwa jambo hili, ofisini kwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Gerald Mweli, anayeshughulikia elimu, aliyelipokea kwa mshangao.

Mweli alianza kwa kuweka bayana msimamo wa serikali kwamba hilo ni kosa kwa mujibu wa miongozo ya elimu iliyopo, huku akiahidi kulifuatilia kwa kina kupata picha kamili kwa ajili ya uamuzi.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu, ambayo ina msingi mkuu kutoka andiko la mwaka 2010, serikali inawajibika katika inachokitamka "kutoa elimu kwa usawa kwa maeneo na makundi mbalimbali".

Vilevile, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na marejeo yake ya mwaka 2014, inapiga marufuku mantiki yote ya uonevu, ubaguzi na unyanyasaji, huku baadhi ya vifungu vyake vikiwa na angalizo la moja kwa moja katika usawa unaotamkwa kwenye Sera ya Elimu.

Sheria hiyo inatoa tafsiri "...'unyanyasaji wa mtoto' maana yake ni ukiukwaji wa haki ya mtoto ambao unasababisha madhara ya kimwili, kimaadili au kifikra ikijumuisha kupigwa, kutukanwa, kubaguliwa, kutelekezwa, kunyanyaswa kijinsia na kazi za kinyonyaji."

Pia inatafsiri maendeleo ya mtoto ambayo inahisiwa katika mkasa huu yanakiukwa, ikiwa na matamshi: "...ni mchakato wa mabadiliko ambao kwao mtoto anaweza kujitawala kimwili, kiakili, kihisia na uwezo wa kipaji katika kumwendeleza katika kila nyanja na kumwezesha kukabiliana na mazingira".

Je, ni zipi haki za mtoto zinazotetewa hata nchini hivi sawa zimetawala pande tofauti kupitia msukumo wa wanaharakati, jamii na serikali? Kifungu cha 5(1) na (2) cha sheria hiyo kina maelezo: "Mtoto atakuwa na haki ya kuishi kwa uhuru bila ya ubaguzi wa aina yoyote; mtu hatambagua mtoto kwa misingi ya jinsia, tabaka, umri, dini, lugha, maoni ya kisiasa, ulemavu, hali ya kiafya, mila, kabila, uasili wa mjini au kijijini, kuzaliwa, hali ya kijamii na kiuchumi, ukimbizi au kwa misingi mingine."

Vilevile, Kifungu cha 8(1) cha sheria hiyo kinaendeleza haja ya wajibu wa mtu yeyote akiwamo mzazi au mlezi mbadala ambayo mara nyingi inajumuisha hata shule wanapomlea mtoto, kumtunza mtoto huyo katika mustakabali muhimu kama wa afya; kinga; elimu; chakula; malazi; mavazi; mwongozo; uhuru; na haki ya kucheza na kupumzika.

## TANGAZO

# UZINDUZI RASMI WA BENKI YA BIASHARA YA TANZANIA (TCB)



*Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB), Bw Sabasaba Moshingi (katikati), akiteta jambo na Mkurugenzi wa Masoko wa benki hiyo, Bw Deogratius Kwiyukwa (kulia), wakati wakitoa maelezo mafupi kwa mgeni rasmi, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe Dkt Mwigulu Lameck Nchemba (kushoto), kabla ya uzinduzi wa benki hiyo mpya jijini Dar es Salaam wiki hii.*



*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt Mwigulu Lameck Nchemba (aliyeketi) na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Serikali ya TCB, Bw Sabasaba Moshingi, wakiteta jambo kabla ya uzinduzi wa benki hiyo mpya.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya TCB, Dkt. Edmund Mndolwa (kushoto), akiwa pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Bw Sabasaba Moshingi (katikati) na Kaimu Msaidizi wa Kamishna toka Wizara ya Fedha na Mipango, Bi Janet Hiza (kulia), wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi, Mhe Dkt Mwigulu Lameck Nchemba, wakati wa uzinduzi wa benki mpya ya serikali inayoitwa Tanzania Commercial Bank.*



*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe Dkt Mwigulu Lameck Nchemba, akiteta jambo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya TCB, Dkt Edmund Mndolwa, wakati wa uzinduzi wa benki mpya ya serikali ya TCB kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam Jumatano wiki hii.*




*Mgeni rasmi katika uzinduzi wa benki mpya ya serikali, Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe Dkt Mwigulu Lameck Nchemba (wa pili waliosimama kulia), pamoja na wageni waalikwa wakiangalia kikundi cha ngoma asili kabla ya hafla ya uzinduzi wa Benki ya Biashara ya Serikali iliyofanyika JNICC Dar es Salaam.*




*Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe Dkt Mwigulu Lameck Nchemba (wa pili kushoto) akizindua rasmi Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB) katika hafla iliyofanyika Jumatano kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.*

Nipashe
MWANGA WA JAMII




# Umakini watakiwa pazia Ligi Kuu Bara likifungwa

**PAZIA** la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 linatarajiwa kufungwa kesho kwa timu zote 18 zinazoshiriki ligi hiyo kushuka dimbani kwenye viwanja mbalimbali nchini kucheza mechi zao za mwisho. Hata hivyo, timu hizo zitashuka dimbani zikiwa na malengo tofauti maana tayari bingwa wa msimu ameshapatikana, na si mwingine ni Simba ya jijini Dar es Salaam ambayo iko chini ya Kocha Mkuu Mfaransa, Didier Gomes anayesaidiana na Suleiman Matola, kiungo na nahodha wa zamani wa timu hiyo.

Mbali na Simba, Mwadui FC yenyewe imeshashuka daraja na itashuka dimbani kesho kuwakabili Polisi Tanzania katika kukamilisha ratiba kwa sababu matokeo yoyote watakayopata hayatabadili hatima yao. Timu nyingine zitashuka dimbani kusaka ushindi kwa ajili ya kuweka heshima maana matokeo yoyote watakayopata katika mechi za kesho hayatabadilisha nafasi ambazo wapo katika msimamo, lakini nyingine zikishuka viwanjani kuchukua pointi tatu ambazo zitawanusuru na janga la kushuka daraja.

Lakini zipo timu ambazo mbali na kujiombea ushindi, pia zitahitaji kuona 'wabaya' wao walioko kwenye janga la kushuka daraja wakipoteza mechi ili wao wabaki kwenye nafasi salama.

Ili mechi zote zichezwe na kumalizika salama na kwa haki au 'Fair Play' kama ilivyozoelekwa, ni lazima Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kwa kushirikiana na Bodi la Ligi kuweka au kuongeza wasimamizi kwa sababu kwa kuhakikisha upangaji wa matokeo hauchukui nafasi kwenye mechi hizo za lala salama.

Endapo hakutakuwa na 'mchezo mchafu' katika mechi hizo za kufunga pazia la msimu, tunaamini timu ambazo zitashuka daraja zitakuwa ni zile ambazo zimeshindwa kujinasua na zile ambazo zitabakia, zitakuwa ni timu ambazo zilipambana na kurekebisha makosa yake.

Kuruhusu upangaji wa matokeo uwepo katika mechi hizi la kumaliza msimu, kutachafua mazuri yote yaliyoonekana tangu raundi ya kwanza mpaka ya 33 ambayo ilichezwa juzi, huku ikitajwa kuwa moja ya ligi bora barani Afrika, mafanikio ya Simba iliyofika hatua ya robo fainali kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa yakiakisi. Tunafahamu ushindani wa timu umeonekana kuongezeka zaidi katika mzunguko wa pili, lakini udhamini mnono wa bilioni 225 uliotangazwa na Azam Media mwezi uliopita ukiziamsha klabu zilizokata tamaa kwa kuongeza nguvu kwenye mapambano kwa sababu zinafahamu fika msimu ujao utakuwa na neema.

Mbali na TFF kujiimarisha katika mechi hizi za kufunga msimu, umefika wakati viongozi, wachezaji na kila mmoja akajipanga kutekeleza majukumu yake kwa weledi ili kujiepusha na adhabu ya faini au kufungiwa kujihusisha na mpira wa miguu na hapo kujiondoka kwenye mfumo wa soka.

Tunawakumbusha waamuzi kutokubali kutumika katika dakika hizi za lala salama na kuhakikisha wanachezesha mechi kwa kufuata sheria 17 za mchezo huo unaopendwa na mashabiki wengi duniani.

Tunaamini mechi zikichezwa kwa weledi, kila klabu inavuna kila inachostahili lakini pia ikawe fundisho kuelekea msimu mpya kwa timu zilizobakia na zile ambazo zimepanda daraja kwa mara ya kwanza. Mpira wa miguu unahitaji uwekezaji, umefika wakati kila anayeshiriki katika mchezo huu akawatendea haki wawekezaji ambao wanatoa fedha zao kwa kutekeleza majukumu yanayomhusu kwa kiwango cha juu kwa ajili ya kujitangaza yeye binafsi, klabu au nchi pale atakapopata nafasi ya kwenda kuliwakilisha taifa kwenye michuano ya kimataifa.

Ni ukweli bado safari au kiwango cha timu zetu kiko chini, na ili tufike kule zilipo timu za Waarabu au Magharibi, hatuhitaji kusubiri miujiza, ni kila mdau kufuata misingi iliyoweka na siku moja, ndoto na kilio cha Watanzania kuona taifa lao linashiriki mashindano makubwa au nchi inatoa mchezaji kwenda katika ligi kubwa zilizoendelea zinatimia. Karibu Mbeya Kwanza, karibu Geita Gold katika msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



Na barnabas Maro

# Bidii ya mja haikidhi njaa

**JUHUDI** za binadamu hazimalizi haja zake. Hii ni methali yenye maana kuwa binadamu hawezi kuzitegemea bidii au jitihada zake peke yake. Ni lazima autegemee uwezo wa Mungu, ambaye ndiye Muumba wa yote.

Wahenga walisema "Mungu ni Mwalimu (mjuzi) wa mbegu za ndimu. Maana yake Mungu anafahamu au ni mjuzi wa kila kitu hata mbegu za ndimu, methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba hamna jambo linaloweza kumshinda Mungu kwani anavifahamu vitu vyote vilivyomo ulimwenguni.

Ndio maana husemwa "Mungu humpa alalaye na akaaye kitako." Maana yake Mungu humpa au kumjalia vitu aliyelala na akaaye kitako. Hii ni methali inayomaanisha Mungu humpa au kumjalia vitu anayelala na akaaye kitako. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba Mungu hana ubaguzi, kwani hawapendelei watu falani.

Wakati wanachama, wapenzi wa mashabiki wa Yanga na Simba wakitamba mitaani kote nchini hata kabla ya timu zao kukutana kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) itakaochezwa Kigoma Julai 25, mwaka huu hali ya ushirikina imeanza kuonekana!

Sikushangaa kusikia uwanja utakaotumiwa na timu hizo pinzani tangu zilipofarakana mwaka 1935 na kuundwa timu ingine iliyoitwa Sunderland ambayo kwa sasa huitwa Simba ya mwaka 1936, kumekuwa na namna fulani ya chuki kati yao hata zikutanapo kwenye michezo yao.

> **Sikushangaa kusikia uwanja utakaotumiwa na timu hizo pinzani tangu zilipofarakana mwaka 1935 na kuundwa timu ingine iliyoitwa Sunderland ambayo kwa sasa huitwa Simba ya mwaka 1936, kumekuwa na namna fulani ya chuki kati yao hata zikutanapo kwenye michezo yao.**

Mfano mzuri ni timu hizo zinapo karibiana kupambana kwenye viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru jijini Dar es Salaam hufanya visa yaani mambo mabaya yasiyopendeza yanayohusu ushirikiana.

Kuanzia hoteli wanazokuwamo hufanywa mazingara usiku kucha huku wale waitwao 'makomandoo' wakiwa uwanjani hulinda vyumba vya timu zao visiingiliwe na wapinzani wao.

Wakati hayo yakiendelea huko wanakokuwa, waganga wa kienyeji wanaostahli kuitwa wachawi huwa kazini wakipanga barabara watakazopitia wachezaji huku wengine wakiwa majumbani mwao wakichoma ubani na kuwaeleza wasaidizi wao mambo ya kufanya barabarani na wanapokuwa uwanjani!

Aidha (vilevile) huelekezwa milango ya kupitia kukwepa milango maalumu iliyoandaliwa kwa wachezaji. Zamani wachezaji wa timu hizo waliambiwa waruke ukuta kuingia uwanjani ili kukwepa ulozi, yaani utendewaji ubaya wa kuwaroga wachezaji waliokusudiwa ili washindwe kucheza itakiwavyo!

Mungu ametupenda kwanza. Upendo wa Mungu mmoja umetajwa katika "maneno" ya kwanza. Toka hapo amri zaweka wazi jibu la upendo ambalo mtu anaitwa kumpa Mungu wake. Imeandikwa: " Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye peke yake."

Yashangaza na kusikitisha jinsi timu zetu za kabumbu zinavyoshiriki na kuamini ushirikina badala ya Mungu Muumbaji wa dunia na vyote vilivyomo-vinavyoonekana na visivyoonekana!

"Bidii" ni jitihada katika kutekeleza jambo lolote; juhudi, ari katika kufanya jambo; idili; juhudi; jitihada; tia hamu au ongeza utashi wa kufanya jambo. Kama mambo au ufanisi ndivyo ulivyo, kwanini hatujibidishi kufanya mambo yetu kwa bidii na kumtegemea aliyetuumba badala yake tunategemea ushirikina?

Ni wazi kuwa ushirikina ni tabia ya kuamini uwezo wa kiumbe kingine juu yako badala ya ule wa Mwenyezi Mungu!

Timu za Simba na Yanga ndizo zilizoanza kuwatumia waganga kwa imani kuwa dawa zao zinaweza kuwanufaisha kila zinapocheza kati yao na pia dhidi ya timu zingine. Imani hiyo sasa yatumiwa na timu zote za kandanda nchini hata zile za mitaani! Mungu ambaye ndiye muumba wa vyote, amesahaulika!

Wahenga walikuwa sahihi waliposema: "Asiyeangalia huishia ningalijua"maana yake mtu asiyeangalia andiko huishia kusema 'laiti ningejua' baada ya kufikwa na jambo. Methali hii yatushauri tuwe watu wa kukanyika au wanaofuata ushauri tunaopewa na wanaotutangulia kwa maarifa au ujuzi kama vile wazee.

Aidha yasemwa: "Bahati ina miujiza lakini haina ahadi." Kwa kawaida bahati huweza kuleta mambo ya ajabu lakini haitabiriki. Maana yake ni vigumu kuitabiri bahati. Kwa hiyo ni vigumu kuitabiri bahati. Hivyo twahimizwa tujitahidi bila ya kutegemea miujiza. Tukijibidisha na kumwomba Mwenyezi Mungu atatusikia na kutusaidia.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784-334 096**

# TANGAZO

## TE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KYELA DISTRICT COUNCIL

## THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE KYELA DISTRICT COUNCIL FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2020

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE - BY NATURE FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 1,317,995,732 | 1,370,406,223 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 1,653,204,216 | 2,457,475,784 |
| Amortization of revenue grants | 11 | 27,405,376,988 | 28,232,844,144 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 10,500,000 | 8,235,000 |
| Finance income | 13 | - | 350,000 |
| Amortization of capital grant | 28 | 2,214,208,185 | 930,484,989 |
| Other revenue | 14 | 53,849,043 | 248,132,574 |
| | | 32,655,134,163 | 33,247,928,713 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 15 | 25,075,166,295 | 26,863,207,889 |
| Supplies and consumables used | 16 | 5,848,130,298 | 1,252,415,108 |
| Maintenance expenses | 17 | 884,794,819 | 521,909,971 |
| Grants and other transfer payments | 18 | 535,539,011 | 3,632,732,625 |
| Provision for Loss and Other Losses | 19 | 426,744,018 | 110,178,147 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 25 | 1,147,176,242 | 1,223,293,538 |
| | | 33,917,550,684 | 33,603,737,279 |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | (1,262,416,521) | (355,808,565) |

These financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 28th September, 2020 and were signed by;-

Ezekiel H. Magehema
CMT Chairperson
Date: 28/09/2020

Gasper Mwanandeje
CMT Secretary
Date: 28/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KYELA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA DISTRICT COUNCIL

### CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020

| | Note | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes and levies | 40 | 1,283,741,831 | 1,304,709,057 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 41 | 1,626,446,439 | 1,907,808,929 |
| Revenue from exchange transaction | 42 | 10,500,000 | 8,235,000 |
| Recurrent grants received during the year | 11 | 26,539,776,008 | 26,983,712,948 |
| Recurrent grants refunded | 11 | (94,158,311) | (64,825,544) |
| Other Revenue | 43 | 53,849,043 | 166,617,793 |
| Change in Deposit Account | 44 | (21,950,590) | 73,033,714 |
| Change in Imprest Account | 45 | (62,803,302) | 77,103,302 |
| Loan Refunded by Women, Youth and Peoples with Disability | 21 | 14,278,900 | |
| Loan Issued to Women, Youth and Peoples with Disability | 46 | (104,647,600) | (28,535,200) |
| **Payments** | | | |
| Employee costs | 47 | (25,197,333,670) | (24,766,270,652) |
| Payments for supplies and consumables | 48 | (2,693,976,715) | (1,769,640,381) |
| Payments for Maintenance expenses | 49 | (871,640,660) | (550,331,010) |
| Grants and Other Transfer Payments | 50 | (535,539,011) | (3,632,732,625) |
| **Net cash from operating activities** | | (53,457,637) | (291,114,670) |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 51 | (969,356,978) | (942,484,989) |
| **Net cash from investing activities** | | (969,356,978) | (942,484,989) |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Development grants received | 38 | 1,514,185,831 | 1,212,186,365 |
| Grants refunded/transferred to RUWASA | 28 | | (290,419,557) |
| **Net cash used in financing activities** | | 1,514,185,831 | 921,766,808 |
| Net increase in cash and cash equivalents | | 491,371,216 | (311,832,852) |
| Cash and cash equivalents at beginning of period | | 1,020,584,405 | 1,332,417,257 |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | | 1,511,955,621 | 1,020,584,405 |

These financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 28th September, 2020 and were signed by:-

Ezekiel H. Magehema
CMT Chairperson
Date: 28/09/2020

Gasper Mwanandeje
CMT Secretary
Date: 28/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KYELA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KYELA DISTRICT COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30TH JUNE, 2020

| | Notes | 2020 TZS | 2019 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 21 | 1,511,955,621 | 1,020,584,406 |
| Receivables and prepayments | 22 | 722,829,455 | 1,012,350,703 |
| Inventories | 23 | 594,972,674 | 3,366,207,613 |
| | | 2,829,757,749 | 5,399,142,722 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 24 | 50,476,367 | 50,476,367 |
| Property, plant and equipment | 25 | 23,898,248,296 | 26,904,269,776 |
| | | 23,948,724,663 | 26,954,746,143 |
| **TOTAL ASSETS** | | 26,778,482,412 | 32,353,888,865 |
| **LIABILITIES** | | | |
| Current liabilities | | | |
| Payables | 26 | 688,009,940 | 1,329,679,691 |
| Employee benefits | 27 | 2,807,194,853 | 2,929,362,227 |
| Deferred income (Grant) | 11 | 236,927,106 | 1,065,024,803 |
| | | 3,732,131,899 | 5,324,066,722 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred Capital (Grant) | 28 | 820,805,992 | 93,902,596 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 4,552,937,891 | 5,417,969,318 |
| **NET ASSETS** | | 22,225,544,522 | 26,935,919,547 |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | 22,170,904,522 | 26,881,279,547 |
| Minimum Compulsory Reserve | | 54,640,000 | 54,640,000 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | 22,225,544,522 | 26,935,919,547 |

These financial statements were authorised for issue by the Council Management Team on 28th September, 2020 and were signed by;-

Ezekiel H. Magehema
CMT Chairperson
Date: 28/09/2020

Gasper Mwanandeje
CMT Secretary
Date: 28/09/2020

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
KYELA

**Opinion**

I have audited the Financial Statements of Kyela District Council, which Comprise the Statement of Financial Position as at 30th June, 2020, the Statement of Financial Performance, Statement of Changes in Net Assets, Cash Flow Statement, and the Statement of Comparison of Budget and Actual Amounts for the year then ended, as well as the notes to the Financial Statements, including a Summary of Significant Accounting Policies.

In my opinion, the accompanying Financial Statements present fairly in all material respects, the Financial Position of Kyela District Council as at 30th June, 2020, its Financial Performance and its Cash Flows for the year then ended, in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act, 1982 (Revised 2000).

**Basis of Opinion**

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Kyela District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General
Dodoma, United Republic of Tanzania.
31st March, 2021

216362402



Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Mohamed Moyo (mwenye miwani ya jua), akitoa maelekezo ya kazi kwa viongozi wa Manispaa ya Iringa juzi, wakati wa ziara yake katika kata zote kukagua miradi ya maendeleo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waondolewa shtaka utakatishaji fedha

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Kampuni ya Jandu Construction & Plumbing Limited, Khairoon Jandu (52), mwanawe na wenzao wawili waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka 11 ikiwamo kughushi saini ya marehemu mumewe kuiba zaidi ya Sh. bilioni 1.033 wameondolewa shtaka la kutakatisha fedha.

Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, alidai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Kassian Matembele, kwamba Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) amewasilisha hati, hana nia ya kuendelea na shtaka la utakatishaji fedha.

Mume wa mshtakiwa Khairoon, Inderjit Sign Jandu ambaye aliyefariki dunia, alikuwa mmiliki wa Kampuni ya Jandu Construction and Plumbers iliyoko eneo la Buguruni Kisiwani.

Wakili Mwanga aliwataja washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni wakili Mohamed Majaliwa (39), mfanyakazi wa Benki ya Exim Ibrahim Sangawe (33) na mtoto Zainabu Tharia (26).

Upande wa Jamhuri unadai kati ya Januari, 2010 na Desemba mwaka 2017, jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote walitenda kosa la kuongoza genge la uhalifu.

Inadaiwa kuwa Januari 16, mwaka 2017, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa Khairoon alighushi saini ya Inderjit Singh G. Jander mumewe ambaye ni marehemu kuonyesha ni nyaraka halali ya muhtasari wa kikao cha Kampuni ya Jandu Construction & Plumbing Limited wakati akijua si kweli.

Ilidaiwa kwamba mshtakiwa huyo Mei 24, 2019, jijini Dar es Salaam, alighushi saini ya Inderjit Singh G. Jandu kuonyesha kwamba ameteuliwa kuwa mkurugenzi wa kampuni hiyo wakati akijua si kweli.

Wakili alidai mshtakiwa Khairoon Mei 25, 2019 jijini Dar es Salaam, alighushi saini ya Inderjit akionyesha kwamba amehamisha hisa katika kampuni hiyo.

Desemba 18, 2018, Khairoon anadaiwa kughushi tena saini akionyesha ni halali wakati akijua si kweli.

Mshtakiwa huyo anadaiwa katika mashtaka mengine kwamba aliwasilisha nyaraka hizo za kughushi Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA).

Khairoon anadaiwa katika tarehe tofauti mwaka 2020, aliiba Sh. 1,033, 860, 100 mali ya Kampuni ya Jandu Construction & Plumbing Limited.

Kwa upande wa mshtakiwa Sangawe, ilidaiwa kwamba, kati ya mwaka 2019 na 2020 akiwa mfanyakazi wa benki ya Exim kwa nafasi ya meneja, alishindwa kutumia mbinu alizo nazo kuzuia utendekaji wa kosa la wizi.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamlika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi Julai 27, mwaka huu. Washtakiwa wote wamepelekwa rumande hadi watakapoomba na kupewa dhamana na Mahakama Kuu.

Wakati huo huo, Mahakama hiyo inatarajia kuanza kusikiliza kesi ya kughushi cheti cha ndoa inayomkabili Khairoon Jandu Julai 28, mwaka huu.

Uamuzi huo ulifikiwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Joseph Rwambano baada ya Jamhuri kudai upelelezi umekamilika.

Katika kesi hiyo, inadaiwa kuwa katika tarehe na mwezi usiofahamika mwaka 2020, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, kwa nia ovu, mshtakiwa aligushi cheti cha ndoa akionesha kuwa ni halali kimetolewa na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA) wakati akijua si kweli.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kwamba mshtakiwa huyo alighushi cheti cha kuzaliwa cha Gurditsingh Jandu akionesha ni halali kimetolewa na Rita wakati akijua si kweli.

Shtaka la tatu ilidaiwa kuwa Juni Mosi, 2020, Kinondoni Dar es Salaam, mshtakiwa huyo anadaiwa kuwasilisha cheti hicho cha kuzaliwa katika Mahakama Kuu katika shauri namba 70 la mwaka 2019.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kwamba Septemba 23, 2020 katika Kituo Kikuu cha Polisi, Khairoon alitoa taarifa ya uongo kwa ofisi wa polisi Bhoke Warioba akijifanya ni mke halali wa Inderjit Jandu na wamezaa mtoto mmoja aitwaye Inderjit Jandu wakati akijua si kweli.

## RC aagiza mahabusu, wafungwa kukingwa na corona

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameliagiza Jeshi la Magereza mkoani hapa, kuwakinga wafungwa na mahabusu dhidi ya virusi vya corona ikiwamo kuweka ndoo za maji na sabuni kwenye maeneo yote.

Sendiga alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara katika Gereza Kuu la Mkoa wa Iringa kwa lengo la kuhamasisha taasisi hiyo kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo. Alisema jangwa na virusi vipya vya corona ni kubwa kama serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inavyotangaza na kuwa mkoa wa Iringa si kisiwa kwa kuwa una mwingiliano mkubwa wa wageni.

Mkuu huyo alitanabahisha kwamba hata katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa kuna wagonjwa wa corona, hivyo tahadhari lazima ichukuliwe. "Niwatake Jeshi la Magereza ndani ya mkoa wa Iringa kuendelea kuwalinda wafungwa na mahabusu dhidi ya janga la corona kwa kuhakikisha mnaweka maji na sabuni katika milango yote ya magereza ili wafungwa, mahabusu na hata watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya magereza kunawa mikono yao mara kwa mara," alisema.

Mbali na maji na sabuni, alisema bado uongozi wa magereza unapaswa kuangalia uwezekano wa kutafuta barakoa kwa ajili ya wafungwa na mahabusu wanapokwenda mahakamani ili kujikinga na ugonjwa huo.

Sendiga alisema ofisi yake itaendelea kuwaomba wadau mbalimbali, akiwamo mganga mkuu wa mkoa wa Iringa kutafuta barakoa kwa ajili ya wafungwa na mahabusu ili wavae wanapotoka kwenda mahakamani au kwenye shughuli za nje.

Pamoja na agizo hilo, Sendiga alisema changamoto mbalimbali ambazo ameelezwa na Mkuu wa Magereza mkoa wa Iringa ikiwamo ya kuboresha mfereji wa umwagiliaji Pawaga ili kuongeza kasi ya uzalishaji wa mazao ya chakula, ataendelea kuzifanyia kazi.

Alisema zile ambazo ziko ndani ya uwezo wake, atazitatua na zilizo nje ya uwezo wake atazifahamisha mamlaka husika.

Awali, Mkuu wa Magereza wa Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Mathias Makama, alisema magereza ya mkoani Iringa yanakabiliwa na msongamano wa wafungwa na mahabusu.

# Wajifungua kwa mwanga wa tochi za simu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAJAWAZITO katika kijiji cha Lusala, Ludewa mkoani Njombe, wamelalamikia adha ya kujifungua kwa kutumia mwanga wa tochi za simu kutokana na ukosefu wa umeme.

Kutokana na adha hiyo, wameiomba serikali kuwapelekea huduma ya nishati ya umeme katika zahanati ya kijiji hicho.

Wakizungumza na Nipashe juzi baada ya mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo hilo, Joseph Kamonga, baadhi ya wanawake hao walisema pindi wanapofuata huduma hasa ya uzazi majira ya usiku, wamekuwa wakiazima taa, maarufu kama washawasha, ambazo huwa zinazima mapema, kutumia tochi za simu.

Mmoja wa wanawake hao, Rebecca Chaula, alisema zahanati ya kijiji hicho haina umeme hali inayowafanya wakati mwingine kutumia mwanga wa simu.

Alisema pia hata maji ya moto kwa ajili ya kusajisafisha, hulazimika kwenda katika zahanati hiyo na mafuta ya taa kwa ajili ya kuchemsha vifaa vyao.

"Usiku ni giza tunahangaikia na vimwanga vya simu. Sasa kama ni mjamzito na unataka kujifungua, lazima uje na taa yako, mafuta ya taa pamoja na simu au utafute hayo mawashawasha (taa ndogo za umeme wa jua) ambayo yanakodiwa kwa Sh. 500 lakini hayakai muda mrefu yanazima," alisema Chaula.

Naye Letisia Mtega alisema: "Cha kwanza tunahitaji mwanga kwa sababu kwenda kujifungua hospitalini ni gharama. Lazima uwe na taa zile kubwa za umeme wa jua ambazo ni Sh. 15,000. Kama huna ndiyo ukaazime hayo mawashawasha. Maji tunanawa ya baridi na huduma zingine zinashindwa kutolewa kwa sababu ya kukosekana kwa umeme."

Diwani wa Lupanga, Minicus Mganwa, alikiri kuwa zahanati hiyo haina umeme licha ya jitihada mbalimbali walizofanya ikiwamo kuweka umeme wa jua ambao nao haukudumu kwa sababu uliharibika.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Dk. Stanley Mlay, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kwamba wamejipanga kuwaingizia umeme kwa gharama za halmashauri.

"Hiyo ni mojawapo ya zahanati ambazo mwaka huu wa fedha tutawaunganishia umeme kwa sababu mapato yao ya kijiji ni kidogo," alisema Dk. Mlay.

"Kwa mwaka 2020/21 tuliweka bajeti ya kuunganisha umeme zahanati tano za Iwela, Igalu, Ilela, Luilo na



# Watakiwa kuandikisha wenye mahitaji maalum

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa elimu mikoa na halmashauri nchini, wametakiwa kuhakikisha watoto wote waliobainika kuwa na mahitaji maalum wanaandikishwa katika shule husika kama ilivyoshauriwa na wataalamu.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Migeha Julius, alisema hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya kuwatunuku vyeti wahitimu wa mafunzo ya elimu jumuishi yaliyoandaliwa kupitia mradi wa elimu jumuishi na Kanisa la Pentekoste Tanzania (FPCT).

Alisema watoto hao waliobainika wenye mahitaji maalum wanashindwa kufikia malengo na ndoto zao za kupata elimu bora wanayokusudiwa na hiyo inachangiwa na kutoandikishwa kwa wakati kwa kuzingatia aina na kiwango cha ulemavu alio nao mtoto.

"Hivyo viongozi wa ngazi za mkoa na halmashauri wahakikishe watoto hao wanaandikishwa kwenye shule stahiki kama ilivyoshauriwa na wataalamu wa elimu ili wafikie malengo yao kama ilivyo kwa watoto wengine," alisema.

Aidha, aliwataka walimu waliohitimu mafunzo hayo kuwahudumia ipasavyo watoto hao ili wafanye vizuri kwenye masomo yao.

"Serikali iko tayari kutoa ushirikiano wa dhati katika kuhakikisha mnatekeleza shughuli za miradi ya maendeleo kwa ajili ya makundi maalum likiwamo kundi la watu wenye ulemavu, hivyo tunawakaribisha na milango iko wazi kwa ajili ya kushirikiana katika shughuli za maendeleo," alibainisha.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau inaandaa mpango utakaowezesha kutenga baadhi ya shule za msingi zinazohudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum, ili zijengewe mabweni kwa ajili yao.

"Pia serikali imepanga kuendesha mafunzo kazini kwa walimu waliopo katika kila shule kuhusu dhana ya elimu jumuishi ili kuwawezesha kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika mfumo jumuishi kwa ufanisi zaidi."

"Hii na pamoja na kuhakikisha vifaa na visaidizi ikiwamo vya kujifunzia na kufundishia, miundombinu rafiki ya shule inaboreshwa kwa kuzingatia aina ya ulemavu, kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum vinapatikana kwa wakati na kuimarisha huduma za kiafya kwa upande wao zinaimarishwa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema mkakati wa serikali ni kuona watoto wenye ulemavu wanapatiwa fursa bora ya kielimu.

# Jafo anusa harufu ya rushwa utoaji vibali nyumba starehe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, amebaini kuna watu walipewa vibali kinyume cha utaratibu na kusababisha kelele na mitetemo kwenye makazi ya watu.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye kituo cha Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Jafo alisema baada ya wizara nane kuja na mkakati wa udhibiti wa kelele na mitetemo kwenye makazi ya watu hasa katika maeneo ya nyumba za starehe na ibada, wananchi wamekuwa na mwamko wa kutoa taarifa hali hiyo ilivyo kero kwao.

"Kuna changamoto tumeipata hivi karibuni kuna watu walipewa vibali kinyume na utaratibu, mtu amepewa Class 'A' apige muziki saa 24 wakati ni baa ya wazi, zingine zimejengwa kwenye makazi ya watu," alisema.

Alibainisha kuwa suala hilo limefanywa na baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kutoa vibali ambavyo vya baa za wazi lakini wamepewa class 'A' kinyume cha utaratibu.

"Hapo sasa unafikiria mtu huyu aliwekewa mazingira gani hadi kutoa kibali cha aina hii? Yawezekana ni rushwa. Hata kama mtu amepewa kibali na sauti inazidi kiwango kinachotakiwa, mfano hivi karibuni nilivyokwenda jijini Mwanza nimekutana na kesi ya aina hiyo anatakiwa kufuata sheria na kanuni," alisema.

"Watanzania watuelewe tunafanya hii kazi kwa maslahi yao na kujiepusha kuwa na watoto wasio sikia kwa sababu ya kuathiriwa na kelele na mitetemo," aliongeza na kusema kwa sasa ofisi yake imeelekeza utoaji wa vibali ufuate sheria, taratibu na kanuni.

"Mtaalamu atakayefanya kinyume cha kanuni tutafuatilia watu waliopewa kinyume cha utaratibu. Inawezekana wamefanya ushawishi, tutachunguza walipataje vibali bila kuendana na masharti. Tunataka utii wa sheria kuwalinda Watanzania hasa watoto wadogo," alisema.

Hata hivyo, Jafo alipongeza wale wenye kumbi za starehe ambao wameweka vizuia sauti nje.

"Kuna wengine baa za wazi kuna midundo hadi nyumba zinapata ufa. Sasa tumewataka wawe na vipima sauti na kusiwe na kero ambazo zitasababisha madhara kwa jamii inayozunguka eneo husika," alisema.

Alisema wataalamu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha watu wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa.

"Baada ya kutoa ripoti za usumbufu na kelele, chini ya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan muda sasa wa kusikilizwa umekuwa mkubwa ili kuondoa changamoto kwenye maeneo yao.

"Hizi kelele zimewekwa katika frequency maalum na kuna vifaa maalum vya kupima kelele, na mtu mwenye kumiliki eneo la starehe anatakiwa kuwa na kipima sauti na kama imezidi aweze kupunguza," alisema.

Alibainisha wataalamu kwasasa wanatoa elimu ya matumizi ya kifaa cha kupima sauti maeneo ya viwanda, nyumba za starehe na kuna muda wa usiku na mchana.



Maofisa wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) makao makau, wakiongozwa na Kanali David Mziray (kushoto), wakiwa katika mazungumzo na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Huduma kwa Majeshi ya Ulinzi na Usalama cha Benki ya NMB, Ally Ngingite (kulia), walipotembelea ofisi za NMB makao makuu, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Halmashauri zapewa mchongo mapato ya ndani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI zimetakiwa kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ili kujitegemea angalau kwa asilimia 10 ya bajeti kwa mwaka badala ya kutegemea serikali kuu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, alipokuwa akifungua mafunzo kwa watendaji wa serikali wa mkoa huo yaliyoandaliwa kupitia mradi wa usimamizi bora wa fedha za umma (GFG).

Dk. Mganga alisema hatua hiyo itachangia kuchochea maendeleo kwa wananchi.

"Viongozi tupo hapa hii ni fursa, serikali ya Ujerumani imeona ije kutusaidia katika suala zima la kukusanya mapato yetu ya ndani. Tunajua lengo la serikali ni kuhakikisha kila halmashauri inajitegemea angalau kwa asilimia 10 ya mapato yake," alisema.

Alibainisha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinategemea halmashauri kwa kiwango kikubwa sana.

"Katika mafunzo haya wanasheria wetu watajengewa uwezo ili kuwa na sheria ndogo kwenye halmashauri kudhibiti ukusanyaji na matumizi ya fedha zinazokusanywa.

"Tumeshiriki kwenye semina nyingi na tukija kupima tulichokipata kwenye semina katika matendo hatupati. Kwenye hili tuchukulie semina hii kipekee tunafundishwa jinsi gani ya kuibuka na vyanzo vipya na kuimarisha vyanzo vilivyopo," alisema.

Alisema Jiji la Dodoma bado halikusanyi mapato vizuri hasa kwenye tozo ya huduma.

"Mapato ya Jiji yameshuka kutoka Sh. bilioni 72 hadi nusu yake. Hiyo inaonyesha tulikuwa tunategemea chanzo kimoja tu cha mapato ambacho ni ardhi," alisema.

Alisema jiji linapaswa kupewa elimu kwa kuwa lina vyanzo vingi vya mapato lakini limejikita kwenye ardhi.

"Kuna mambo chungu mzima hatujazingatia vizuri na tukakusanya kwa ufanisi ili kujitegemea, Jiji la Dodoma lilipaswa kujitegemea kwa asilimia 100 lisichukue fedha Serikali Kuu ili ihangaike na halmashauri maskini," alisema.

Hata hivyo, alisema anaamini kupitia semina hiyo Jiji litapiga hatua kwenye makusanyo yake.

Mshauri Mwandamizi wa Mradi wa GFG, Dk. Stephen Ehrentraut, alisema mradi huo utatekelezwa kwenye mikoa sita ambapo kwa Dodoma ni kwenye Halmashauri ya Jiji la Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.





# Wakulima wang'aka tozo miamala ya simu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) na kampuni ya simu ya Zantel zikiwahakikishia wakulima na wafanyabiashara wa karafuu uhakika kuwa na mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki ni wa uhakika na salama kwa fedha zao, baadhi wamelalamikia makato ya muamala kwa njia ya mtandao wa simu yalivyoongezeka.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima wa karafuu walisema tozo mpya za makato hayo zitasababisha hasara kubwa kwao.

"Kilo moja ya karafuu kwa daraja la kwanza ni Sh. 14,000, sasa tukisema niuze karafuu zangu kilo moja na malipo yangu kulipwa kwa njia ya miamala ya simu kiwango nitakachotoa kitakuwa hakilingani na bei niliyouza," alisema Makame Ali, mkulima wa karafuu katika Kijiji cha Donge, Kaskazini Unguja.

Alisema kutokana na tozo hiyo ya miamala ya simu, watarejea utamaduni wao wa zamani wa kuhifadhi fedha zao katika vibubu.

"Tunafahamu kuwa kuna huduma za kibenki lakini huku kwetu vijijini huduma hizo zaidi ziko mjini. Sasa mimi nimeshauza karafuu zangu kweli nitoke huku nende mjini nikaweke pesa benki? Si bora nihifadhi katika kibubu au njia zetu za asili za kuhifadhia fedha ikiwamo chini?" Alihoji.

Awali, wakizungumza katika kipindi maalum katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC TV) ZSTC na Zantel waliwataka wakulima kukubaliana na njia hiyo ya malipo kutokana na ubora na faida yake kwa wakulima na serikali. Akizungumzia ubora na usalama wa mfumo huo wa malipo kwa njia ya kielektrokini, Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Baucha, alisema njia hiyo ni salama na ya uhakika.

"Imefika wakati wa kuachana na malipo taslimu ambayo si salama. Fedha lazima ziwe salama. Njia hii ya malipo ya karafuu kwa njia ya elektroniki ni salama zaidi kwa fedha," alisema Baucha.

Alisema njia hiyo ya elektroniki itawawezesha wakulima wa zao la karafuu kutumia huduma za EYZPESA kwa matumizi na malipo mbalimbali viganjani mwao. Naye Mkurugenzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu, Ali Suleiman, alisema ZSTC na wakulima wa karafuu wamefanya kazi katika mazingira magumu kwa kipindi kirefu kutokana na malipo taslimu katika vituo vya ununuzi wa karafuu.

"Shirika lilikuwa linakwenda na fedha nyingi ambapo ilihitaji kuwa na ulinzi mkubwa na wakulima walikuwa wanaondoka na fedha nyingi taslimu vituoni. Hali hii haikuwa salama," alisema.

Alisema kwa kipindi kirefu shirika lilitamani matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika malipo ya karafuu, hivyo kuja kwa mfumo huo hivi sasa watendaji watafanya kazi kwa weledi na uhakika zaidi.

Alisema kuwa baadhi ya wakulima wanaonyesha kuwa na wasiwasi na njia hiyo ya malipo lakini akasema ZSTC kwa kushirikiana na Zantel itaendelea kutoa elimu kwa wakulima.




Mwenyekiti wa Taasisi ya Asma Foundation, Asma Mwinyi (kulia), akipokea msaada wa boksi 36 za taulo za kike zenye thamani ya Sh. milioni 2.9 kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Confidence Product ya Dar es Salaam, Fanta Kaijage, katika hafla iliyofanyika Maisara mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Tumbatu ya Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tume ya Uchaguzi yapata bosi mpya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar. Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi wa wakurugenzi kwa baadhi ya taasisi wakiwamo wanne ambao wote ni sura mpya.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Salum, aliyoitoa kwa vyomboo vya habari, Rais Mwinyi amemteua Khamis Kona Khamis kuwa Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Pia amemteua Mohamed Ame Makame kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii na Said Mtumwa Faki kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji na Mpigachapa Mkuu wa Serikali Zanzibar (ZAGPA).

Mwingine aliyemteua ni Mshauri Khamis Abdulla kuwa Mkurugenzi wa Mipango ya Rasilimali Watu katika Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Uteuzi huo ulianza jana.

Katika hatua nyingine, Dk. Mwinyi juzi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Ethiopia nchini Tanzania, Yonas Yosef Sanbe, ambaye alifika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kujitambulisha na kuhimiza nchi za Afrika kushirikiana katika kuimarisha biashara.

Dk. Mwinyi alisema kuwapo kwa safari za Shirika la Ndege la Ethiopia katika nchi nyingi za Afrika, ikiwamo Tanzania, kutaimarisha zaidi ushirikiano wa kibiashara na sekta zingine.

Pia Rais Dk. Mwinyi alimpongeza Balozi huyo kumpa taarifa juu ya hali ya kiuchumi, kisiasa na kijamii inavyoendelea nchini humo pamoja na hatua zinazochukuliwa na serikali ya Ethiopia katika kuhakikisha mafanikio yanapatikana.

Naye Balozi Sanbe alisema uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Ethiopia ni wa kihistoria ambao umeasisiwa na Hayati Rais Julius Kambarage Nyerere na Hayati Mfalme Haile Selassie.

Balozi Sanbe alisema uhusiano huo na ushirikiano bado unaonekana kwa kuacha alama na jina la Mfalme Haile Selassie linatumika Zanzibar na bado kuna Shule ya Sekondari ya Haile Selassie kwa upande wa Zanzibar pamoja na barabara ya Haile Selassie, Dar es Salaam.

Balozi huyo alimweleza Rais Mwinyi kwamba nchi yake inathamini sana uhusiano na ushirikiano huo wa kihistoria na ameahidi itaendelea kushirikiana na Tanzania ikiwamo Zanzibar katika kuanzisha nyanja zingine za ushirikiano ikiwamo biashara.

Alisema ushirikiano na uhusiano kati ya Zanzibar na Ethiopia unahitajika zaidi na hata utamaduni wa wananchi wa Ethiopia na Zanzibar umeshabihiana kwa kiasi kikubwa, hivyo kuna haja kwa pande mbili hizo kuutunza ili uzidi kuleta manufaa.

# Wapigwa jeki hedhi salama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Confidence Products ya Dar es Salaam, imekabidhi taulo za kike maboksi 36 kwa Taasisi ya Asma Foundation ya Zanzibar kwa ajili ya wasichana na wanawake visiwani Zanzibar.

Akipokea taulo hizo jana, Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Asma Ali Mwinyi, alisema taulo hizo atazitoa kwa wanafunzi wa kike wa Shule ya Tumbatu Kaskazini Unguja ili kuhudhuria masomo bila vikwazo wakati wa hedhi.

Alisema wakati watapotoa taulo hizo kwa wasichana 400 wa kisiwa cha Tumbatu na pia watapewa elimu ya hedhi salama ili wanapoingia katika hali hiyo kutokuwa na aibu na kutokuwa wachovu.

Kwa mujibu wa Asma, mahitaji ya taulo za kike ni makubwa zaidi vijijini ambako elimu ya matumizi yake inahitajika ili kuwawezesha wanafunzi kwa muda wote kuhudhuria masomo shuleni.

"Wapo wanafunzi wanapoingia katika hedhi huwa hawahudhurii masomo na wengine huona aibu kutokana na hali wanayokuwa nayo kipindi cha hedhi, hivyo wakati wa kuwapa taulo hizi kwanza tutawapa elimu ya hedhi salama na jinsi ya kutumia taulo," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kuna baadhi ya mila hasa vijijini, wanawake wanapokuwa katika hedhi huwa wanatengwa na kutoshirikishwa katika baadhi ya huduma za kijamii.

"Tunashukuru tumepokea taulo za kike ambazo katika awamu ya kwanza tunatarajia kuzipeleka kwa wanafunzi wa Shule ya Tumbatu ili wazitumie katika kipindi wanachopata mabadiliko ya hedhi na isiwe kikwazo cha kuhudhuria shule," alisema. Pia alisema matarajio ya baadaye ya taasisi yake ni kufikisha huduma hizo katika kisiwa cha Pemba chenye visiwa vidogo ndani yake vipatavyo sita ili kukabiliana na changamoto kama hizo ambazo zinawakabili wanafunzi.

Naye Mkurugenzi wa kampuni ya Confidence Products, Fanta Kaijage, alisema mikakati yao kuhakikisha mtoto wa kike anakuwa salama muda wote na hedhi, hivyo isiwe sababu ya kikwazo cha kukosa elimu.

Alisema kwa mujibu wa utafiti waliofanya kwa baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara, mahitaji ya taulo za kike ni makubwa ambayo kukosekana kwake ni kikwazo kwa wanafunzi wa kike kushindwa kuhudhuria vizuri shuleni.

"Tumekuwa tukitoa taulo za kike katika mikoa ya Tanzania Bara. Sasa tumefika Zanzibar kwa ajili ya kuwafikia watoto wa kike wenye mahitaji ya aina hiyo," alisema huku akibainisha kuwa taulo hizo zilizotolewa zina thamani ya Sh. milioni 2.9.




# MARUFUKU MISS WORLD

# Miss Tanzania mtovu wa nidhamu

HATIMAYE sababu ya Miss Tanzania, Rose Manfere, kuenguliwa kushiriki katika shindano la Dunia imefahamika rasmi.

Azama Mashango ambaye anatoka kampuni ya The Look Company Limited, ambao ni waandaaji wa shindano la urembo nchini, amesema mrembo huyo amekosa nidhamu.

Mashango amesema kuwa Rose alikiuka baadhi ya vifungu vya mkataba wa makubaliano yao kwa kufanya baadhi ya vitendo vya utovu wa nidhamu hali iliyosababisha kunyang'anywa nafasi ya uwakilishi wa nchi katika msimu wa 70 wa shindano Miss World la mwaka huu.

Hata hivyo, nafasi yake itajazwa na mshindi wa pili, Juliana Lugumisa.

Hata hivyo, Baraza la Sanaa Taifa (BASATA), limesema halijaridhia na halijakubaliana na maamuzi ya kumuengua Miss Tanzania kwenye ushiriki Miss World mwaka huu mpaka pale kamati ya Miss Tanzania itakapotoa sababu za msingi na kuzithibitisha.

Shindano la Urembo la Dunia linalotarajiwa kuanza kufanyika mwezi Desemba 16, mwaka huu katika jiji la San Juan, nchini Puerto Rico kwenye ukumbi wa Coca-Cola Music.

Chanzo: EATV


BASI SAWA

## Marioo aungana na mastaa wengine



MWANAMUZIKI nyota Marioo, ataungana na mastaa wenzake kwa kutoa albamu zao kwa kishindo mwaka huu. Marioo ambaye anatamba na kibao chake "Mama Amina" amesema kupitia ukurasa wake wa Instagram, kwamba mwezi Septemba mwaka huu, albam hiyo itakuwa tayari. Kutokana na sababu za kibiashara, mwanamuziki huyo hajataja nyimbo na wasanii aliowashirikisha kwenye album hiyo.

## Utata Miss Tanzania wazidisha hofu



UTATA wa kunyang'anywa taji kwa Miss Tanzania, Rose Manfere, kunazidisha mijadala katika mitandao ya kijamii kutokana kuwapo usiri kuelezea nini chanzo cha kuchukuliwa hatua hiyo.

Mtangazaji wa kipindi cha Nirvana ya East Africa Televisheni, Deo ameingilia mjandala huo akisema mrembo huyo hana ujauzito.

Akizungumzia hilo kwenye shoo ya DADAZ inayorushwa na EATV, amesema jibu litapatikana lakini Miss huyo hakuvuliwa taji. "Miss Tanzania hajavuliwa taji ila taarifa iliyopo hatawakilisha mashindano ya Miss World, pia sio mjamzito labda ni masuala ya mkataba ndio taarifa nilizo nazo, ukiwa mrembo hutakiwi kuwa mjamzito au kuolewa ukiwa na taji".




# Kajala mwambie Paula anawakera watu

BAADHI ya watu wametilia shaka malezi ya Paula kutoka kwa mama Kajala Masanja, kutokana na kauli binti yake kuwakera mashabiki wa Harmonize.

Hata hivyo, mchora tattoo The Lion Ink, amemtetea Paula kwa kusema kauli yake iliyosikika wakati mama yake akifutwa tattoo yenye jina la Harmonize, ilikuwa bahati mbaya na pengine alikerwa na matukio ya nyuma.

"Ile kauli ya tunatoa uchafu ilitoka kwa Paulah, wakati anarekodi video mimi na Kajala tulikuwa hatujui kinachoendelea, kwa mimi nilivyoelewa ile tattoo ni kitu ambacho kilikuwa kinamkera sana kwa hiyo kwake hata ile H aliona kama takataka ndiyo maana nikaitoa ile H nikaweka tattoo ya Uaridi" amesema The Lion Ink

Mengine zaidi aliyoyazungumza mchora tattoo huyo wakati anafuta tatoo ya H kwa Kajala tazama kwenye video.



# Diamond basi inatosha!

UNAWEZA kusema ni wiki ya Diamond Platnumz! Hii inatokana na wiki nzima mwanamuziki huyo kuwa katika bata la aina yake kufurahia mafanikio yake ya kimuziki.

Diamond ambaye amekulia katika umaskini kule Tandale, na kisha kuibukia katika ukwasi wa kifedha kiasi ambacho sasa anamiliki gari la kifahari aina ya Rolls Royce ya rangi ya blue.

Kupitia mtandao wake wa Instagram, msanii huyo ameweka picha na video fupi akiwa na wasanii wenzake wa hapa nchini na Afrika Kusini, wakifurahi na kula pamoja katika hoteli za nyota tano.

Aidha mwezi mmoja uliopita staa huyo wa muziki alinunua gari mpya aina ya Cadillac Escalade Sky Captain inayodaiwa ina thamani ya Sh. milioni 811.



## Mume Aliyekimbia: Mwisho wa kutamani kuku na yai lake

**Na Adam Fungamwango**

NI tabia iliyojengeka kwa baadhi ya wanaume kuwatia mimba wasichana na kuwakimbia.

Leo tutaiangalia filamu ya 'Mume Aliyekimbia', ambayo inaelezea kisa cha kusikitisha kilichotokana na kosa la mtu mmoja ambaye anakuja kufanya kosa lingine kwa mara ya pili linaloleta matatizo kwenye familia yake na yeye mwenyewe.

Imechezwa na Suleiman Barafu, Stanley Msungu, Riyama Ally, Najma Ally na Catty Rupia na wengineo. Inaanza kuonyesha kuwa Barafu anaishi vema na mkewe Catty.

Shetani anamwingia na kuingia kwenye penzi na msichana mwanafunzi wa sekondari aitwaye Najma. Penzi linanoga kiasi cha mkewe kujua kuwa mumewe ana matatizo kwa sababu alibadilika tabia.

Riyama ambaye ni mama wa Najma kutokana na kuletewa pesa na binti yake akawa hajui binti yake aendelee na masomo au aendelee na mchezo wake mchafu. Najma anapata mimba. Inamchanganya mama na Barafu mwenyewe.

Najma kuitoa hataki na Barafu ana mke. Binti anajiona bora azae ili awe mke wa Barafu.

Barafu anandaa mbinu kabambe na rafiki yake Msungu. Mbinu yenyewe ni kumuua Najma. Kwa sababu amekataa kutoa mimba na yeye ni mwanafunzi kitu ambacho kilimtisha Barafu kuwa anakaribia kuingia kwenye mdomo wa jela.

Msungu anamuua Najma, lakini anakamatwa alipokuwa anakwenda kutupa maiti iliyokuwa ndani ya gari.

Hata hivyo anasema kuwa yeye si mhusika ila alitumwa. Anaachiwa kwa sharti moja tu la kumkamatisha mhusika.

Barafu katika pitapita yake anakutana laivu na Riyama, mama yake marehemu Najma. Wanakumbukana. Miaka mingi iliyopita kwenye kijiji kimoja, alimpachika mimba Riyama na kukimbia. Alijifungua mtoto wa kike akamwita Najma. Kumbe Barafu alimpa mimba binti yake. Lakini alifanya njama ya kumuua.

Polisi na Msungu wanakwenda kumchukua Riyama, wakimweleza kuwa wamempata muuaji wa binti yake. Wanakwenda nyumbani kwa Barafu na kumkamata. Riyama alipoona sura ya Barafu na kujua kuwa yule ndiye alimpa mimba binti yake na pia kumuua anaanguka chini na kuzirai.

## Wanatesa kama baba zao

**Na Adam Fungamwango**

MAJI hufuata mkondo. Mtoto wa nyoka ni nyoka. Hiyo ni misemo ya kiswahili inayoonyesha kuwa mara nyingi watoto hufuata tabia au mambo ambayo wazazi wao wanayafanya.

Ingawa si mara nyingi, au lazima iwe hivyo, lakini wanayoyafanya baadhi ya watoto wanaakisi kile ambacho wazazi wao wanakifanya.

Leo tunawaangazia wasanii wa muziki wa kizazi cha sasa ambao wamerithi vipaji kutoka kwa baba zao.

Yaani baba zao walikuwa wanamuziki huko nyuma na baadaye watoto waliowazaa wakaja kuwa kama wao.

**TX MOSHI 'JUNIOR'**

Huyu ni mtoto wa mwanamuziki wa zamani wa bendi ya Msondo Music, Tx Moshi William. Anaitwa Tx Moshi 'Junior', lakini jina lake halisi ni Hassan Moshi.

Kwa sasa ni mwanamuziki wa bendi aliyokuwa akipigia baba yake. Tx Moshi 'Junior', ni msanii mwenye vipaji vingi kwani kabla ya kurithi kazi ya baba yake aliwahi kujiingiza kwenye tasnia ya kuigiza na kucheza filamu kadhaa, kiasi cha kumfanya hata baba yake naye acheze baadhi ya filamu chache.

Mtoto wa Moshi, alijiingiza rasmi kwenye muziki wa dansi baada ya kifo cha baba yake mwaka 2006.

Kwenye bendi ya Msondo, Tx Junior ni mwimbaji kama alivyokuwa baba yake.

**PAPY KOCHA**

Ni mwanamuziki ambaye anajulikana sana na kizazi cha sasa na cha kati. Mwanzoni mwa miaka ya 2000, aliwika akiwa na bendi za FM Academia, TOT Plus na Achigo Band.

Alifungwa jela mwaka 2004, kabla ya kutolewa kwa msamaha wa Rais Dk. John Magufuli mwaka 2017. Bado anaendelea na muziki.

Papy Kocha yeye amerithi kazi ya baba yake Nguza Mbangu 'Viking', aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Maquiz Du Zaire kwenye miaka ya '70 hadi mwanzoni mwa miaka ya '90.

Nguza ambaye kwa sasa anajulikana sana kwa jina la 'Babu Seya', aliwahi pia kupigia bendi ya Sambulumaa na kuanzisha bendi yake ya Achigo kabla kufungwa jela na watoto wake akiwamo Papy Kocha 2004 na kusamehewa 2017. Hata baada ya kutoka kifungoni, wote Baba na Mwana wanaendelea na mambo ya muziki.

Wakati Papy Kocha aliimba, baba yake ni mpiga gitaa la solo, bass na kuimba pia.

**BANANA ZORRO**

Banana Zorro ni mmoja wa wasanii nyota kabisa wa kizazi kipya kwenye muziki wa bongo fleva. Sidhani kama kuna kijana wa kizazi cha sasa hamjui. Ametunga na kuimba nyimbo nyingi sana maarufu ambazo zinapendwa na zitaendelea kupendwa. Huyu pia amerithi kazi ya baba yake.

Ni mtoto wa mwanamuziki iliyokuwa bendi ya JKT Mafinga, maarufu kama 'Kimulimuli' iliyokuwa na maskani yake mjini Iringa, Zahir Ally Zorro.

Baadaye mzee huyo alijiunga na bendi ya Sambulumaa na kutunga kibao kilichopendwa na wengi 'Cleopatra'.

Hadi leo Zahir anaendelea na shughuli za muziki kama mwanaye. Wote wana uwezo wa kupiga gitaa na kuimba.

**KASSIM MGANGA**

Anajulikana kama msanii wa bongo fleva, lakini kwa siku za karibuni amekuwa akiimba nyimbo zenye vionjo ya Pwani. Nyimbo zake za sasa nyingi anazifanya kwa mtindo wa mduara hivi.

Huyu pia amerithi kipaji hicho si kutoka kwa baba yake, tu bali pia mama yake.

Baba yake ni Hemed Mganga, aliyekuwa mwanamuziki aliyepigia bendi mbalimbali kama Atomic Jazz, Urafiki Jazz, Uda Jazz, Orchestra Makassy na Legho Stars, huku mama yake akiwa ni mwimbaji mwenye vikundi vya taarab Tanga, vikiwemo Bandari Modern Taarab na Coast Modern Taarab.

Mzee Hemed alikuwa ni mpiga gitaa la kati 'rhythm', huku mtoto wake Kassim yeye ni mwimbaji.

**OCHU SHEGGY**

Naye pia ni mmoja wa wasanii wa kizazi kipya ambaye amerithi kazi kutoka kwa baba yake.

Ochu, ni mtoto wa mwanamuziki wa zamani wa bendi za Super Rainbow, Vijana Jazz, Washirika Tanzania Stars na Bantu Group, Eddy Sheggy.



# Maisha yote sawa, omba uzima





MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Moesha Boduong, ametangaza kufilisika katika akaunti yake ya benki baada ya kununua gari la kifahari aina ya Range Rover.

Kulingana na msanii huyo, kwa sasa hana kitu na hawezi kufanya jambo lolote, lakini bado ana furaha kutokana na kupata gari hilo ambalo ilikuwa ndoto yake.

Katika video iliyosambaa katika mitandao ya kijamii alisikika akisema "Siwezi kuwa na pesa katika akaunti yangu ya benki, zote nimenunulia gari."



## Wendy kuwa mtulivu kwa hili

Wendy Shay, amekuwa hana furaha baada ya kuwa na hofu kutokana na baadhi ya wasanii chipukizi wa Nigeria kujihusisha kimapenzi na mastaa wa Ghana.

Akihojiwa katika redio moja, mwanamuziki huyo amekiita kitendo hicho ni aibu, kwani ikiacha ikiendelea kunaweza kuleta matatizo kutokana na mastaa hao kuwatumia ili kupata uraia wa Nigeria.

"Utamwona mwigizaji chipukizi anajihusisha kimapenzi na staa mmoja maarufu wa Ghana, tumepata gharama kubwa kwa watu kutoka nje," amesema.

## Daniel hongera zako

MSANII wa filamu kutoka Nigeria, Daniel Etim-Effiong, amewatangazia mashabiki wake kuwa hivi karibuni anatarajia kuitwa baba.

Akitumia akaunti yake ya Instagram, amewaambia mashabiki wake kuwa yeye na mke wake wanajiandaa kupata mtoto.

Mwanamuziki huyo ameposti picha akiwa katika chumba cha uzazi pamoja na mwanamke mwenye ujauzito, jambo ambalo mashabiki wake wanaamini tayari mke wake amejifungua.





## Kizz Daniel watoto pacha si haba

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Oluwatobiloba Daniel maarufu kama Kizz Daniel, amesema amebarikiwa kupata watoto mapacha watatu.

Kizz Daniel, ametaja majina ya watoto hao kuwa ni Jelani, Jalil, na Jamal ambao walizaliwa miezi kadhaa nyuma lakini kwa kusikitisha alimpoteza Jamal siku nne baadaye.

"Mungu alinibariki wavulana watatu, Jamal, jalil na Jalan, siku nne nilimpoteza Jamal, lakini nilimwahidi nitakuwa baba bora zaidi kwa kaka zake," ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.

## Toto Dikeh ajianika baada ya upasuaji

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Tonto Dikeh, amekuwa na mwonekano tofauti na ule wa awali baada ya kufanyiwa upasuaji wa kurekebisha viungo.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, msanii huyo aliweka picha mbalimbali zikiwa za kipindi cha nyuma na baada ya upasuaji na kuonekana yupo katika utofauti mkubwa.

"Baadhi ya watu wananiuliza kwa nini nimefanya upasuaji, vizuri sana kwa kutumia picha hizi nitakuwa nimejibu maswali yenu," ameandika.



# Mabasi ya abiria yanaweza kuwa mwarobaini ulaji chakula bora

NA GAUDENSI MNGUMI




Vijana wabunifu wanachama wa ANSAF wakishiriki mkutano wa taifa wa mifumo ya chakula, ili kuandaa ajenda za Tanzania kwa ajili ya mkutano wa awali UN utakaofanyika Roma Julai 26 hadi 28, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MKUTANO wa awali wa Umoja wa Mataifa (UN) wa mifumo ya chakula duniani unaopewa jina la The Pre-Summit of the UN Food Systems Summit, unaolenga kuangalia namna chakula kilivyo nyenzo muhimu ya kufanikisha utekelezaji wa malengo 17 endelevu, unafanyika nchini Roma kuelekea mwishoni mwa Julai mwaka huu.

Katika mkutano huo wa utangulizi UN itaonyesha nia yake ya kujitolea kuendeleza usawa na haki kwa kila binadamu kupata chakula kazi itakayofanikishwa na kuboresha mifumo ya chakula ili asiachwe hata mmoja.

Mkutano unaowaleta pamoja vijana, wakulima, makundi asilia, Azaki, watafiti, sekta binafsi, mawaziri wa kilimo, mazingira, afya, lishe uchumi na fedha, unataka kuwe na mifumo ya endelevu ya chakula kuanzia uzalishaji, uvunaji, usafirishaji, usindikaji hadi kuliwa ili iwezesha kila mmoja kupata chakula salama na bora.

Wakati Tanzania ikielekea kwenye mkutano huo, serikali na vijana wabunifu wadau wa mwamvuli unaounganisha mashirika ya kiraia yanayoshughulika na kilimo (ANSAF) wanakutana jijini Dodoma kuangalia jinsi taifa litakavyofanikisha kupata mifumo bora ya chakula kufikia malengo endelevu.

Katika jukwaa linalokutanisha wadau kutoka mashiriki ya kitaifa na kimataifa kama VI-Agriforestry, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), Wizara ya KIlimo, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na mashirika ya vijana.

Mkurugenzi wa Shirika la Wajasiriamali Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUGECO), Revocatus Kimario, akizungumza katika jukwaa hilo anasema wakati umefika wa kuwa na kampeni endelevu za kitaifa kuzungumzia na kuelimisha wananchi umuhimu, ulazima na kujua ni kipi chakula bora na mifumo ya endelevu ya chakula.

Anasema kufuhamu mifumo bora ya chakula ni muhimu ili kuwawezesha wananchi kwa wakati wote kupata chakula cha kutosha, kilicho salama na chenye lishe bora na kwamba kufahamu suala hilo kutawafungua wananchi kuzijua athari za kukosa chakula bora ambazo ni pamoja na uwezo mdogo wa kufikiri kwa watoto au udumavu wa mwili na akili.

Na kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Kilimo kiwango cha udumavu nchini ni asilimia 32 na hicho ni chanzo cha udhaifu watoto ambao wanaathirika kutokana na uwezo mdogo wa kufikiri pamoja na kufanya kazi ili kumudu maisha yao.

Kama watoto kwenye taifa watashindwa kufikiri inamaanisha wanafamilia, jamii na nchi itakuwa na maendeleo duni kwani kwenye nguvu kazi na kitaaluma, anasema Kimario anapozungumza na Nipashe.

Anasema ukosefu wa chakula husababisha maradhi kuanzia kwa wajawazito, watoto kuugua mfano malaria, kuhara, magonjwa nyemelezi, ukosefu wa damu na kulazwa muda mrefu huku kazi za maendeleo kusimama na maradhi huleta vifo.

### VITAMBI MARADHI

Kimario anasema lishe duni huleta udumavu lakini ulaji usio bora husababisha vitambi (viriba tumbo) na magonjwa kama kisukari kwa watoto wanaozaliwa bila insulin na hata wakubwa ambao insulin inashindwa kufanyakazi na kutaka kuwe na kampeni za kitaifa kuleta mabadiliko.

### KAMPENI ZA MAGARI

Anasema: "Utafiti nilioufanya ni wa mabasi ya abiria. Haya yanaweza kutumiwa kuwapelekea watu ujumbe wa lishe bora. Kwenye mabasi kuna muziki, vichekesho, mahubiri na sinema. Wenye mabasi waweke burudani hizo lakini, waongeze ujumbe wa lishe , uzalishaji, usafirishaji, utunzaji, usindikaji na ulaji chakula bora," anashauri

Anashauri kuandaa ujumbe wa kitaalamu kuhusu chakula, lishe bora, athari za kukosa chakula, usalama kwenye uzalishaji, usafirishaji, usindikaji na ulaji duni.

"Mathalani, wastani wa mabasi 400 yanafika katika kituo cha Mbezi iwe kutoka ama kwenda mikoa kila siku. Kila moja lina abiria 60 kwa hiyo ni wastani wa watu 24,000 wanapanda mabasi hayo. Kwa mwezi ni wastani wa abiria 720,000 na kwa mwaka watafikia wasafiri 8,640,000 na kwamba kwa mujibu wa Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS) kuna takribani watu watano kwa kila familia, hivyo iwapo abiria milioni 8.6 watasikia ujumbe huo na kuupeleka nyumbani wanafamilia milioni 43.2 kwa mwaka watakuwa wameusikia," anasema na kushauri kuingiza simulizi za chakula bora kuanzia sasa.

Anasema mabasi ya mijini na daladala nayo yana mchango huo na yanafaa kutumiwa pia.

### WASANII WAHUSISHWE

Kimario anawageukia wasanii, anawaambia imetosha wameimba nyimbo za mapenzi na mipasho na sasa waanze kutoa tungo zenye maudhui ya lishe bora, mifumo endelevu ya chakula ili kubadilisha mifumo duni ya ulaji.

Anawashauri waelimishe jamii mfano ianze kula lishe bora yenye viini muhimu, kutumia mboga, matunda, maziwa, kunywa maji ya kutosha mara kwa mara kuepuka kula mafuta mengi au vyakula vya kukaanga muda wote watasaidia kubadilisha mawazo kuhusu lishe bora.

Aidha, anashauri jamii kutumia mapango yanawekwa mitaani kutangaza taarifa za ulaji bora badala ya hata ikibidi kuyaweka pembeni ya matangazo ya waganga wa kienyeji ambayo yanapatikana kila kona mijini na pengine hata vijijini.

### KAMPENI KWENYE SIMU

Kimario anawageukia wenye simu za mkononi akipendekeza hata miito (ringer) iwe na mkakati wa kitaifa kuleta ujumbe wa lishe bora, kuielezea, kuisisitiza na kutaja hasara, faida za kula au kukosa mlo bora. Kuzungumzia matumizi bora ya viuatilifu na virutubishi pamoja na kujali badala ya kutupa chakula.

### MBINU MBADALA

Mkurugenzi wa SUGECO anataka jamii kujikita kwenye kuchanganya vyakula mfano, unga wa ngano na viazi lishe.

"SUGECO tunatumia teknolojia ya 'Puree' kuandaa mchanganyiko huo... Chemsha viazi kwa mvuke, chukua sufuria weka maji kidogo, weka wavu na panga viazi juu ya wavu visiguse maji. Funika na jani la mgomba kubakiza mvuke ndani. Vikiiva ponda na pima gramu 300 viazi na 700 unga wa ngano andaa chapata au mkate wenye mchanganyiko huu," anasema Kimario.

Anakumbusha kuwa uchanganyaji huo, huongeza ladha, lishe na virutubisho na kuwa na vyakula mbadala kupunguza mazoea.

### VYAKULA VILIVYOSAHAULIKA

Mtaalamu huyo wa kilimo na lishe bora, anawakumbusha Watanzania kuanza kula vyakula vilivyosahaulika au vyakula asilia. Anautaja mchicha pori, mchunga, mboga chungu, mlenda pori, nyanya asilia, mapera, zambarua na jamii zote za matunda, mboga, mimea ambazo zinapatikana vijiji lakini siyo kwenye 'super market'.

### MABADILIKO SHULENI

Kimario anasema kusoma na kujifunza habari za chakula bora ndiyo mwanzo wa mabadiliko na kushauri shule za msingi na sekondari kuanzisha mashamba darasa la kilimo cha mazao asilia yakiwamo matunda na mboga zinazopatikana kwenye maeneo yao.

"Tuwafunze watoto kuvua siyo kula samaki. Wajue ukulima na uzalishaji wa chakula walimu mijini na vijini waanze kuwafundisha watoto kulima na kuandaa vyakula. Wawafunze sayansi, siasa na stadi za kazi na kilimo ili wajue umuhimu wa ulaji wa chakula bora.

# Vigogo hawa wa Afrika ‘wamechinjwa’ kwa mtutu

## •Wamo Karume, Deby, Kabila

Na Christina Mwakangale

KINAPOTOKEA kifo kwa kuuawa kiongozi wa taifa, jamii huwa na udadisi mkubwa, wengi wakihoji namna gani mkuu wa nchi atafikiwa na kukatishwa uhai, licha ya ulinzi alionao.

Ndani na nje ya Afrika wakuu wa nchi wawili wameuawa mwaka huu, akiwamo Idris Deby wa Chad na Jovenel Moïse wa Haiti, aliyeuawa mwanzoni mwa mwezi huu.

Viongozi waliouawa wakiwa madarakani ni 118 duniani, kwa mujibu wa ripoti kutoka Marekani ya Military Medicine (Vol. 163).

Mwaka 1965 hadi 1996 viongozi wakuu wa nchi 261 walifariki, kati yao 118 walifariki wakiwa madarakani huku asilimia 44 ya wakiuawa, wengine144 walifariki baada ya kutoka madarakani, lilisema jarida hilo.

**KUPIGWA RISASI**

Rais wa Haiti Jovenel Moïse, aliyeuawa kwa kushambuliwa kwa risasi kwenye makazi yake, mjini Port-au-Prince ni mfano wa karibuni wa viongozi wakuu wa nchi zaidi ya 100 kuuawa katika kipindi cha miongo saba.

Matukio hayo yanatokea duniani mara nyingi huripotiwa katika nchi za Mashariki ya Kati, Asia ya Kusini na Afrika.

John Kennedy wa Marekani, Park Chung-hee wa Korea Kusini, Francois Tombalbaye wa Chad, Hafizullah Amin wa Afghanistan, Anwar Sadat wa Misri na Thomas Sankara wa Burkina Faso ni kati ya waliouawa.

Barani Afrika, tukio la kwanza la mauaji mwaka huu ni la kushambuliwa kwa risasi Idriss Deby wa Chad, aliyoiongoza nchi hiyo kwa miaka 30 hadi Aprili mwaka huu.

Aliuawa wakati akiongoza majeshi ya nchi hiyo kukabiliana na waasi waliokuwa wanataka kumwondoa madarakani.

Ilikuwa ni siku moja baada ya kutangazwa mshindi wa uchaguzi mkuu, akipata asilimia 80 ya kura zote katika uchaguzi uliofanyika Aprili mwaka huu.

Deby aliingia madarakani kwa mapinduzi na kumfurusha aliyekuwa rais na mkubwa wake jeshini, Hissene Habre, urafiki wao uliyumba baada ya Habre kumtuhumu Deby, kutaka kumpindua.

Deby akatimkia Libya kisha Iraq, akarudi Chad 1989 na kumfurusha Habre.

Sheikh Abeid Aman Karume wa Zanzibar, Rais wa kwanza wa Zanzibar na Makamu wa kwanza wa Rais wa Tanzania, ni kiongozi mwingine aliyeuliwa kwa risasi.

Anaendelea kuheshimika visiwani humo kwa jitihada zake za kuileta Zanzibar pamoja, pia kuviunganisha visiwa hivyo na Tanganyika na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa la Tanzania.



Rais Muamar Gaddafi (katikati) na walinzi wake. Alikuwa anapendelea kulindwa na wanawake. **PICHA: MTANDAO**

Sheikh Karume aliuawa kwa kupigwa risasi katika makao makuu ya Chama cha Afro-Shirazi (ASP) visiwani mjini Zanzibar, Aprili 7, mwaka 1972.

Kiongozi huyo hatasahaulika katika historia ya ukombozi wa visiwani humo kutokana na misingi aliyowajengea Wazanzibar.

Muammar Gaddafi, Rais wa Libya, ubabe wa kivita ulimsaidia kuingia madarakani mwaka 1969, alikamatwa na kuteswa kabla ya kuuawa Oktoba 2011, kufuatia mapigano yaliyoitwa ‘Battle of Sirte, kati ya wanajeshi wanaomtii na wasiomtii kiongozi huyo.

Haikuthibitishwa iwapo alijiua kwa bastola, ila Waziri Mkuu wakati huo, Mahmoud Jibril, ndiye alitangaza kifo, akisema amefariki kwa majeraha ya risasi bila maelezo zaidi.

Laurent-Desire Kabila, Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), alikuwa rais wa tatu wa taifa hilo, wakati huo likiitwa Zaire.

Aliongoza nchi kuanzia 1997 hadi alipouawa Januari 2001, baada ya kuingia madarakani kwa kumfurusha Mobutu Seseseko.

Kabila alibadilisha katiba na kurejesha jina la DRC na kulifuta jina la Zaire, aliuawa akiwa ofisini na walinzi wake waliokuwa wakiitwa kadogoo kabla ya kukimbizwa Zimbabwe kwa matibabu.

Kifo kilitangazwa Januari 18, ingawa Waziri wa Afya wa wakati huo, Leonard Mamba aliyekuwa chumba cha pili cha ofisi wakati shambulio likitekelezwa alieleza kwamba Kabila alifariki papo hapo.

Wiki moja baadaye mwili wake ulirejeshwa DRC kwa mazishi ya kitaifa, kabla ya mtoto wake Joseph Kabila, kumrithi na kuwa rais wa nchi hiyo, siku 10 tangu baba yake auawe. Watu 130 walihusishwa na njama za kifo chake akiwamo mmoja wa wapwa zake na kuhukumiwa adhabu mbalimbali.

Mwingine ni João Bernardo Vieira, rais wa Guinea Bissau, aliongoza nchi hiyo kwa vipindi vitatu tofauti kuanzia 1980 hadi 1999, kasha 2005 hadi 2009.

Mwaka 1980, Vieira aliiongoza Guinea-Bissau kwa miaka 19 na akashinda uchaguzi mkuu wa vyama vingi wa mwaka 1994, vita ya wenyewe kwa wenyewe mwaka 1998 hadi 1999 vilisitisha utawala wake na kutimkia ng’ambo.

Mwaka 2005 alishinda uchaguzi wa rais. Hata hivyo miaka minne baadaye, Machi 2009, akauawa na wanajeshi wake saa chache baada ya kuuawa kwa mkuu wa majeshi Jenerali Batsta Tagme Na Waie.

Samuel Doe wa Liberia, mwanajeshi, nguli wa vita, aliyeingia madarakani kwa mtutu wa bunduki akiwa na wanajeshi wenzake 17 na kuwa rais kwa miaka 10 kuanzia 1980 hadi 1990.

Anadaiwa kuhusika na ukiukaji na uvunjifu wa haki za binadamu. Alitajwa kukandamiza zaidi wapinzani kiasi cha kuzua kasheshe la kupingwa na kukataliwa wazi hali iliyotikisa serikali yake.

Uchaguzi wa 1985 ulimpa ushindi ikidaiwa ulikuwa wa udanganyifu na kuanzia hapo akaanza kuandamwa na wapinzani akiwamo Yormie Johnson na Charles Taylor, aliyeongoza kundi la National Patriotic Front, kumwondoa madarakani.

Kukazuka vita kati ya kundi la Taylor na Doe, iliyowakimbiza maelfu ya raia kwenda kutafuta usalama nchi jirani, Ivory Coast.

Akiwa njiani kukimbia nchi Septemba 1990 akiwa na walinzi takribani 60, walivamiwa na kundi la Yorme Johnson na akauawa siku iliyofuata.

Yupo Jenerali Ibrahim Baré Maïnassara, Rais wa Niger, ni mwanajeshi anayetokea kabila la dogo la Maouri katika jamii yenye watu wengi ya Hausa aliyeitawala Niger kwa miaka mitatu kati ya mwaka 1996 mpaka 1999.

Kupitia katiba iliyoondoa utawala wa kijeshi mwaka 1991, kufika Machi 1995 Maïnassara akawa Mkuu wa Majeshi na uchaguzi wa bunge wa Januari mwaka 1995, uliosababisha mvutano mkubwa kati ya rais wa wakati huo Mahamane Ousmane na bunge lililokuwa na wabunge wengi wa upinzani chini ya Waziri Mkuu Hama Amadou.

Maïnassara alitishia kuwa hawezi kuona nchi inadorora kwa sababu rais na waziri wake mkuu wanasigana, akashika hatamu mpaka alipouawa na walinzi wake Aprili 1999, akielekea kupanda helikopta katika jiji la Niamey, kwenda nje ya nchi.

HABARI KITAIFA

# Wapigana vikumbo mikopo ya pikipiki

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

ZAIDI ya vijana 100 katika Jimbo la Masasi Mjini, wamejitokeza kuomba mkopo wa pikipiki 25 katika ofisi ya mbunge wa jimbo hilo, Geoffrey Mwambe.

Ofisi ya Mbunge mapema mwezi huu, ilitoa matangazo kuwa itakopesha kwa masharti nafuu pikipiki 25 kwa vijana walioko ndani ya jimbo hilo, ili kujiajiri na kujipatia kipato kupitia kazi yao ya bodaboda ambayo ni maarufu kwa vijana kwa sasa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya vijana hao ambao wamejitokeza kuomba mkopo huo, walisema wanampongeza mbunge kwa kutaka kuwapatia fursa hiyo ya kiuchumi.

Abdallah Bakari, mmoja wa vijana hao, alisema kundi la vijana ndilo kundi ambalo kwa sasa linakabiliwa na tatizo la ajira, hivyo mbunge ameona ni vyema kuwasaidia vijana kuondokana na tatizo hilo kwa njia ya mkopo wa pikipiki.

Alisema vijana wameamua kujitokeza kwa wingi kuomba mkopo huo kwa sababu wanakabiliwa na tatizo la ajira na mitaji ya kuanzisha biashara, hivyo fursa hiyo ni muhimu kwa kuwa hivi sasa dukani pikipiki inauzwa kwa Sh. milioni 2.5, jambo ambalo vijana wengi hawana fedha hizo.

Salum Athumani, mkazi wa Masasi, alisema kwa taarifa walizonazo kutoka ofisi ya mbunge ni kwamba pikipiki zinazokopeshwa ni 25 lakini vijana waliojitokeza kuomba ni zaidi ya 100 hali inayoonyesha kwamba vijana wana uhitaji na mkopo huo kwa kiasi kikubwa.

Alisema utaratibu wa ukopaji wa pikipiki hizo kutoka ofisi ya mbunge umewavutia vijana wengi kujitokeza kwa wingi na kuomba licha ya idadi ya pikipiki kuwa ndogo.

"Mkopo huu kwetu ni tunu tofauti ile inayotolewa na taasisi zingine binafsi za mikopo ambazo zimekuwa na riba kubwa, hivyo vijana wengi tunaogopa kukopa lakini huu ni rafiki ndio tumeomba ingawa hatujui ni nani atapata," alisema Athumuni.

Katibu wa Mbunge, Iman Mkumbo, alisema ni kweli ofisi ya mbunge imetangaza mikopo ya pikipiki kwa vijana wa jinsia zote lengo likiwa kuona vijana wazitumia katika kujiajiri kupitia kazi ya bodaboda.

Alisema pikipiki hizo zitakopeshwa kwa Sh. 2,050,000 badala ya ile bei ya dukani ambayo pikipiki hizo aina SUNLG huuzwa kwa Sh. milioni 2.5 lakini kutokana na mbunge kuthamini mchango wa vijana katika maendeleo, ameamua kuwakopesha ili waendelee kuleta mchango wa maendeleo kwa taifa na Jimbo la Masasi.

# RC Ibuge ageukia migogoro ya ardhi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, amewaagiza maofisa wa ardhi kutatua migogoro ya ardhi kwa kuwatembelea wananchi badala ya kusubiri migogoro hiyo kuwakuta ofisini.

Jenerali Ibuge alitoa maagizo hayo jana katika kikao kazi cha watumishi wa sekta ya ardhi mkoani Ruvuma ambacho kilishirikisha watendaji mbalimbali wakiwamo wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya na watumishi wengine ngazi ya wilaya na mkoa kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea.

Alisema maofisa ardhi wanapaswa kufanya kazi kwa weledi na kwa kuzingatia maadili ya kazi, kutojiuhusisha kuomba na kupokea rushwa na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu sheria mbalimbali za ardhi.

"Ikumbukwe kuwa baadhi ya migogoro ya ardhi hutokea kutokana na wananchi kutofahamu sheria za ardhi. Kwa hiyo kinachohitajika hapa ni uelewa wa sheria ili wananchi kuzifahamu," alisisitiza.

Pia aliwataka maofisa hao kuendelea kukamilisha kazi zote za urasimishaji wa makazi holela katika halmashauri zote za mkoa na kwamba kipaumbele kiwe katika Manispaa ya Songea ambako kazi hiyo inafanyika kwa kasi ndogo kulinganisha na wingi wa maeneo yaliyojengwa holela.

Katika hatua nyingine, Jenerali Ibuge aliwataka wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya uwekezaji na yanahitaji fidia, kuendelea kuwa watulivu wakati serikali inatafuta fedha.

Maeneo yanayohitaji fidia yaliyoko Manispaa ya Songea ni Bonde la Mto Ruhila, eneo la EPZA Kata ya Mwengemshindo na Barabara ya By Pass ya Mtwara Corridor.

Katika kikao kazi hicho, RC Ibuge aliwaagiza wanasheria wa halmashauri zote kwa kushirikiana na maofisa ardhi na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kutoa elimu ya namna bora ya kusuluhisha migogoro ya ardhi kwa wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya kata kwa sababu wameonekana kuwa sehemu ya kikwazo katika kutenda haki kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alishauri kuwa ili kutatua migogoro ya ardhi, bajeti ya kupima ardhi iongezwe ili eneo kubwa lipimwe kuepusha matatizo ambayo yanatokana na maeneo mengi kutopimwa.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi (wapili kulia), akipampu maji baada ya kuzindua mradi wa maji wa kisima kirefu katika Shule ya Sekondari Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Tanzania mwenyeji maonyesho utalii EAC

**Na Lusungu Helela,** ARUSHA

TANZANIA inatarajia kuwa mwenyeji wa Maonyesho ya Kikanda ya Utalii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yanayotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu, jijini Arusha.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye Mkutano wa Kisekta wa Baraza la Mawaziri wa Utalii na Wanyamapori wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika kwa njia ya Mtandao, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, aliwaeleza mawaziri hao kuwa Tanzania iko tayari kuwa mwenyeji wa maonyesho hayo.

Waziri Ndumbaro alitoa ombi hilo baada ya Burundi iliyotakiwa kuwa mwenyeji wa maonyesho hayo kutokuwa tayari kuyafanya kwa mwaka huu, hivyo kuahidi kuwa itakuwa tayari mwakani. Hali hiyo ililazimu Tanzania kuomba na kisha kukubaliwa.

Alisema lengo la maonyesho hayo ambayo ni ya kwanza kufanyika kwa nchi wanachama wa EAC, ni kutangaza fursa za uwekezaji katika sekta ya utalii na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika nchi hizo.

Dk. Ndumbaro alisema makubaliano ya kuanzisha maonyesho hayo ni hatua mahsusi kwa nchi wanachama wa EAC kujitangaza badala ya kutegemea kampuni kubwa za utalii kutoka nje kutangaza vivutio hivyo kwa namna zinavyotaka zenyewe.

Akizungumza katika mkutano huo, Dk. Ndumbaro, amewaelezea mawaziri hao kuwa maonyesho hayo ya utalii nchini Tanzania ni hatua muhimu ya kuwatia nguvu sekta binafsi ya kuona namna ya kujipanga upya kurudi katika biashara ya utalii kutokana na ugonjwa wa corona kuitikisa vibaya sekta hiyo.

Alisema corona imedumaza kampuni binafsi na kusababisha wafanyakazi, hivyo kuongeza tatizo la ajira nchini."Kwa vile Burundi imeonyesha kutokuwa tayari, sisi Tanzania tuko tayari kufanya maonyesho hayo kwa mwaka huu ikiwa lengo letu kutuma ujumbe kwa mataifa makubwa kuwa tuko tayari kuwapokea na kuwahudumia watalii," alisema.

Katika hatua nyingine, Tanzania imeendelea kushikilia msimamo wake wa kuomba muda zaidi wa kujiandaa kujiunga kwenye visa ya pamoja ya watalii.

Waziri Ndumbaro aliwaeleza wajumbe hao kuwa suala la visa ya pamoja ya utalii kwa Tanzania ni suala nyeti na linahusisha mamlaka zaidi ya moja katika kufanya uamuzi, hivyo inaomba ipewe muda zaidi kwa ajili ya kufikia maafikiano na mamlaka zingine hususani uhamiaji na usalama.

Alisema suala la visa ya pamoja ya utalii linahitaji makubaliano ya ndani kwanza kabla Tanzania haijaamua kujiunga nayo jambo ambalo mjadala wake wa kuitaka Tanzania kujiunga liliungwa mkono na mawaziri wa kutoka Kenya na Uganda.

Dk. Ndumbaro alisema suala la visa ya pamoja ni muhimu kibiashara lakini linagusa usalama wa nchi, hivyo aliwashauri mawaziri hao liamuliwe na mamlaka zingine ikizingatiwa kuna Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**SELEMANI FAKHI LIKWILITI** anatangaza kupotelewa na kadi ya **BAJAJI** yenye jina la **ABDALAH SALUM NINGA** aina ya **RE** yenye namba za usajili **MC 136 BZG.** Chasis **No.MC2A25BZ6JWL890333,** Engine No. **AZZWJL26435** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/325805/2021.**

116362702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA.**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILINDI**

**Kituo cha KWEDIBOMA Mkoa wa TANGA.**

**Shauri la madai namba 23/21.**

**Jina la mdai DICKSON EMMANUEL MWAFYELA.**

**Jina la mdaiwa JOSHUA KIPARA.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo kwa Joshua Kipara wa Kijiji cha Kwedigole. Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba wewe Joshua na wenzako wawili mnadaiwa na mdai jumla ya sh. 1,555,000 zikiwa ni fidia ya uharibifu wa mazao ya mdai. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 27/7/2021 saa 2.30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. Angalizo: kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 7 Mwaka 2021.

116362502

---

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi NO. 70/2021**

**Ombi la WILBAD KAIZA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu REHEMAELLY MALEKWA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 22/07/2021 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 06/07/2021.

Tarehe 6/7/2021

Sahihi ya Hakimu

116362302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NO 141 YA 2020**

**AHAMDIL ABDULL.............................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ELIA MAGAYA**
**ZAINABU BARNABA**
**JOSHUA ELENEST.........................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA ELIA MAGAYA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 20/07/2021 mbele ya Mh. M. KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 06 mwezi Julai 2021

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

116361902

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY**
**AT DAR ES SALAAM**

**CIVIL APPEAL NO.70 OF 2019**
**(0riginal from civil case no8 of 2018,resident magistrate's court of kibaha at kibaha j.j.mkhoi,RM)**

**CHARLES SALUM KAVISHE..........APPEALANT**

**VERSUS**

**BUNDALA MAULID BUNDALA.............1st RESPONDENT**
**KADRI WAZIRI........2nd RESPONDENT**
**ISAAC MAIGU.......3rd RESPONDENT**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**TO.ISAAC MAIGU,**
**MASHUJAA STREET-SINZA PALESTINP O BOX**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS,**the above mentioned case has been fixed for mention 29th day of july,2021 at 09:00 am before hon. DR J.L.MASABO-judge you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that aforementioned ,the suit will be held and determined in your absence.

GIVEN under my HAND and SEAL of court this 9th day of may,2021

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

216360302

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHINA CIVIL ENGINEERING CONSTRUCTION CORPORATION** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TRAILER yenye namba za usajili **T 316 AGW,** chassis namba **DT 1111.** Yeyote atakayeiona au kuiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/250403/2021.**

116346502

---

**GSP AUCTION MART**
P.o.Box 31088 Dar es Salaam
Tanzania, Tel: + 255 687 638679 +255 654 922892
Sinza Africasana near by sokoni Africasana Block No. 31
Email: gsp.recovering@gmail.com / gsp.recovering@outlook.com

## KUMB No. AFCL/2021/DM/025

**GSP AUCTION MART** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na kampuni ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED S.L. P 40780** Dar es salaam, tunapenda kutangaza mnada wa hadhara wa kuuza Magari kwa njia ya mnada wa magari twaja hapo chini.Siku ya Jumatatu ya tarehe 26/07/2021. Mnada utaanza Saa 5:00 kamili asubuhi katika yadi ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** iliyopo Dar es salaam vingunguti na Mwanza Sinai Mabatini.

| CUSTOMER NAME | MODEL | VEH_NO | LOCATION |
|---|---|---|---|
| MOSES PETER ABDONI | LP 909 BUS | T877 DNN | DAR ES SALAAM |
| ABDALLAH KIBWANA KIBWANA | LP 909 BUS | T351 DPS | MWANZA |
| CCS POWER SOLUTION (T) LTD | LP 909 BUS | T701 DPB | DAR ES SALAAM |
| FILGONA RANGA DUKO | LP 909 BUS | T178 DPE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T678 DNE | DAR ES SALAAM |
| LUKE ASSOCIATE LTD | PRIMA 2523 | T613 DMQ | DAR ES SALAAM |
| SHABAN RAJABU SOUD | LP 909 BUS | T615 DQF | DAR ES SALAAM |
| MAHENDA SOGONI CONSTRUCTION CO. LTD | LPK 2518 TIPPER | T264 DRD | DAR ES SALAAM |
| BARBARA PRAYGOD MAWALLA | ULTRA BUS | T440 DTE | MWANZA |
| MICHAEL WILLIAM KILIWA | LPT 1116 | T533 DSP | DAR ES SALAAM |
| ROSEMARY GERVAS FILIPO | LP 909 BUS | T925 DQF | ARUSHA |
| VITALIS EDWARD KAHISE | LP 909 BUS | T612 DQY | DAR ES SALAAM |

1. Dhamana itauzwa Kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.
5. Kwa yeyote atakayeharibu mnada hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**
**GSP AUCTION MART PO BOX 310088 DAE ES SALAAM. +255 654 922 892, +255 687 638 679**

216362602

---

Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

---

**MOPEH COMPANY LIMITED**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na benki ya **LETSHEGO** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mteja alioshindwa kulipa mkopo wake, mnada utafanyika siku ya jumamosi **Tarehe 31/7/2021** saa nne a nusu asbuhi. Angalia jedwali hapo chini:

| Na | JINA LA MDAIWA | TAWI | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LILLIES DAY CARE CENTRE | TEMEKE | LILIAN KUBAGA | NYUMBA | MBEZ BEACH -MAKONDE | 31/07/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa jinsi ilivyo
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% ya bei ya mnada ya siku ya mnada na asilimia 75% -iliyobakia ilipwe ndani ya siku 14, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
3. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa4.30 asubuh hadi saa 10 alasiri.
4. Gharama za kubadili hati ya umiliki (transfer of ownership) ni za mnunuzi.

**KWA MAWASILIANO:**
**Wasiliana na ofisa wa Mopeh Co. Ltd au**
**Fika ofisi za Akiba zipo ktk jengo la Amani Place, Barabara ya Ohio**
**kwa maelezo zaidi au**
**Piga simu no: 0785 335544 , 0673 335528**
**au no 0755731072**

116363002

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Kwa sababu haiwezekani ndugu wa Morogoro wawe wanamuona usiku anakuja kuwasalimia, halafu washindwe kuwaambia wenzao wa Dar kuwa ndugu yao yuko hai.

Akajua sababu ya ndugu wote kutohangaika na kumuachia yeye tu. Walijua yupo hai salama, salimini. Awali alijua sababu ya kwamba aliandika kijikatarasi kuwa asitafutwe ndiyo maana ndugu hawakuhangaika, lakini sasa alipata kitu kingine pia.

Haikumwingia akilini laini zake zote mbili hazipatikani siku zote, halafu ndugu wake wapo kimya tu.

Aliona kilichobaki ni kuchekecha akili yake nini cha kufanya baada ya hapo. Aliomba Mungu aongozwe zaidi na akili na busara na si nguvu.

Kwanza kabisa hakutaka kuongozana na mlevi yule kwenye shughuli hiyo. Hata hivyo alimheshimu kwa jinsi alivyompa data zote kwa usahihi na uhakika. Lakini alitaka yeye mwenyewe ndiye awe kwenye eneo la tukio.

"Nashukuru sana rafiki yangu kwa kunipa taarifa. Kwa bahati mbaya sana, nimepigiwa simu nahitajika Dar. Hivyo nakwenda mara moja, nitarudi baada ya siku mbili ili tuendeleee kumtafuta." Tom aliongopa.

Aliingiza mfukoni na kutoa noti za shilingi elfu kumi zikawa kumi. Ni shilingi laki moja. Akamkabidhi. Ilikuwa ni kama ndoto kwa Gaga.

"Tutoke tu ukanionyeshe hiyo baa, kabla ya mimi kuondoka."


Gaga alikubali akiwa na furaha moyoni, wimbo mdomoni. Ni miaka mingi sana alikuwa hajashika kiasi hicho cha pesa.

**********************

Akiwa kwenye hoteli aliyofikia. alijitazama kwenye kioo, akatabasamu. Ni kweli alibadilika. Ni kama siyo yeye.

Tangu alipoonyeshwa ile baa ya Mwenda na mlevi Gaga, Tom aliwaza na kuwazua nini afanye. Ndiyo atakwenda kwenye eneo la tukio, lakini ikitokea akimuona mkewe Farida nini atafanya?

Hakujidanganya kama akimkuta kwenye eneo hilo basi atakuja peke yake. Alijiandaa kushuhudia matukio ambayo yatamchoma moyo. Yatamkatisha tamaa. Yatamliza na kumnyima raha.




**Mwanaume anaweza kwenda peke yake, lakini hawezi kumaliza na kuondoka akiwa peke yake. Atapata mpenzi hapo hapo. Au atakaa na muda si mrefu atakuja mpenzi wake walioahidiana naye.**

Lakini lengo lilikuwa pale pale. Ni kujua kwa nini Farida amefanya jambo hili. Kwa nini alikubali kuolewa na yeye. Tena alilazimisha. Kwa nini wiki moja tu baada ya ndoa amemtoroka?

Hilo ndilo lililomfanya ajiingize kwenye kazi ya kuutafuta ukweli, ukiacha ile ya kumsaka mkewe.

Baada ya kuachana na Gaga, alielekea Morogoro mjini na kununua vifaa ambavyo aliona vitamsaidia kukamilisha kazi yake.

Alijibandika ngozi laini kwenye mashavu yake. Haikuwa ngozi halisi. Alivaa ndevu za bandia na kubandika masharafa. Alichukua mawani akavaa. Juu alivaa kofia kubwa ya pama. Siku hiyo alivaa koti kubwa na suruali pana ya kitambaa. Mabadiliko yote hayo yalimbadilisha mwonekano kiasi kwamba hata mama yake mzazi asingemtambua kama angepishana naye njiani.

Alipokuwa na uhakika na hilo, aliamua pia kubadilisha mwendo. Akaamua kuwa atakuwa anachechemea, kama mtu ambaye aliwahi kuumia mguu huko nyuma.

Safari iliianza hadi kwenye baada ya Mwenda. Ni baa iliyoonekana kuwa maarufu na kupendwa na watu wengi Morogoro, kwani ilijaa watu wa kila aina.

Aliingia na kwenda kukaa nyuma ya baa pembeni. Akamkumbuka marehemu kaka yake Julius.

Alikuwa ni askari kwenye kitengo cha upelelezi. Kama ndugu yake aliwahi kummegea baadhi ya mbinu ambazo zingemfanya asiwe kama raia wa kawaida. Zingemfanya kujua nini afanye anapokuwa kwenye hali gani. Nini afanye au akae anapokuwa kwenye gari, baa, hotelini au anapomhisi mtu ambaye ana shaka naye, lakini pia anapomfuatilia mtu mwenye wasiwasi naye.

Na ndiyo maana alianza kutumia mbinu ya kujibadilisha. Hata kukaa nyuma. Alishaambiwa kuwa akiingia hotelini au kwenye baa anachotakiwa kufanya ni kukaa sehemu ambayo ataona mlango mkuu na si kukaa sehemu ambayo ataupa mgongo.

Hii inaweza kumfanya kuepuka au kuhisi hatari ambayo huenda ingetokea baadaye eneo hilo.

Kifupi alijifunza mengi ambayo baadhi alishayafanyia kazi.

Dakika zipatazo 20 tu tangu aingie, waliingia watu wawili ambao aliwahitaji.

Mmoja alimfahamu na mwingine hakumfahamu.

Kidogo akurupuke na kumfuata, lakini akajikumbusha kuwa kuna kazi anatakiwa aifanye.

Alikuwa ni Farida. Mkewe aiyefunga naye ndoa Dar, wiki moja na siku kadhaa tu zilizopita na akaamua kumkimbia.

Aliongozana na mwanaume mmoja mrefu mwembamba, aliyevaa shati la maua, akiwa amechomekea na suruali nyeusi.

Wivu ulimshika. Chozi kwa mbali lilimiminika. "Hivi kweli Farida ndiyo wa kunifanyia hivyo mimi?"

Kwa bahati nzuri au mbaya, walikwenda kukaa kwenye meza zinazokaribiana naye. Wakaagiza vinywaji.

Walikuwa kwa furaha, ingawa si ya kupitiliza. Moja ya kosa ambalo aliliona Tom ni kuwa peke yake.

Kwenye shughuli anayoifanya inayofanana na upelelezi kwa mujibu wa marehemu kaka yake ni kosa kubwa.

Karibu watu wote ndani walikuwa na wapenzi wao. Kitendo cha yeye kuwa peke yake kingeweza kutiliwa shaka kama kungekuwa na mtu mmoja humo ndani mwenye kipaji au ujuzi na mambo ya kipelelezi.

Mara nyingi kwenye baa, wanawake ndiyo wanaweza kuwa peke yao hadi mwisho na wanaondoka, lakini si wanaume.

Mwanaume anaweza kwenda peke yake, lakini hawezi kumaliza na kuondoka akiwa peke yake. Atapata mpenzi hapo hapo. Au atakaa na muda si mrefu atakuja mpenzi wake walioahidiana naye.

Ukiona mwanaume amekwenda baa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Haonekani kuwa na haja hata ya mwanamke. Mawili, ana 'stresi', au kuna kitu amefauta, na hapo wale watu wa intelejensia au siku hizi wanasema kuwa 'waliosomea Cuba', watakuwa wana wasiwasi naye.

Tom alilifahamu hilo. Alijua kama kuna mtu mwenye ujuzi huo anaweza kuwa na shaka naye. Alimwita mhudumu mmoja na kuongea naye kwa dakika kadhaa. Dakika tano baadaye alikuja msichana mwingine.

"Kaka nimekuletea huyu. Ni mhudumu wa baa hii, ila leo yuko 'ofu', amekuja kuleta pesa ya mchezo." Mhudumu alimwambia Tom, akamgeukia mwenzake.

"Tedi huyu mgeni ameomba kampani, hana mtu, kwa hiyo kuwa naye, usiniangushe."

Tedi alikaa kwenye siti ya pili kutoka kwa Tom. Sasa walionekana kama wapenzi kamili. Na hilo ndilo alilihitaji. Nao waliagiza viywaji.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# VARANE, Trippier wakaribia United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inakaribia kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 68 kwa walinzi wawili, Raphael Varane na Kieran Trippier, kwa mujibu wa ripoti.

Mashetani wekundu hao tayari wameshakubali uhamisho wa pauni milioni 72.9 kwa Jadon Sancho - ambapo tangazo la kusajaliwa kwake rasmi kutangazwa hivi karibuni baada ya kufuzu vipimo vya afya.

Na sasa United wanapanga kuimarisha safu yao ya ulinzi na nyota hao wawili ndio wametajwa kuwa kwenye rada zao.


Mazungumzo yamefanyika kati yao na wawakilishi wa mlinzi wa Real Madrid, Varane na gazeti la Sun limeripoti kwamba, mshindi huyo wa kombe la Dunia ameshakubali kuhamia Old Trafford.

Uhamisho wa Varane kwenda kwa mashetani wekundu hao unaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri na kwamba anatarajiwa kusaini mkataba wa miaka mitano, ingawa bado hawajafikia makubaliano ya ada na Real.

Miamba hao wa Hispania, wana nafasi ndogo sana ya kumbakiza mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, ambaye ameonyesha wazi nia ya kutaka kuondoka.

United wana matumaini kwamba, ada ya pauni milioni 50 itatosha kwa Real kumuachia Varane na ripoti hiyo imedai kuwa pia Trippier anatarajia kutua kwao wiki ijayo.

Mlinzi wa kulia wa Atletico Madrid, Trippier anataka kurudi kwenye Ligi Kuu ya England na ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 18 na kituo chake kitakachofuata ni Man United.




# Arsenal kumsajili Abraham wa Chelsea

**LONDON, England**



ARSENAL imeripotiwa inawania kumsajili straika wa Chelsea, Tammy Abraham, kwa mujibu wa Telegraph.

Chelsea wanaonekana wanataka kumuuza Abraham kipindi hiki cha majira ya joto baada ya straika huyo kushindwa kupata namba kikosi cha kwanza chini ya kocha Thomas Tuchel aliyechukua mikoba ya Frank Lampard, Januari.

Chelsea inataka kulipwa kiasi cha pauni milioni 40 kwa Abraham, huku pia West Ham na Aston Villa zimeonesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23.

Arsenal wanataka kumsajili Abraham, ambaye utotoni alicheza kwa washikabunduki hao na alikuwa shabiki mkubwa wa Thierry Henry wakati akikua.

Hata hivyo, ripoti zinadai kwamba, Arsenal itahitaji kuuza kwanza wachezaji kabla ya kuhitaji kufikia ada ya pauni milioni 40 inayotakiwa na Chelsea.

Arsenal tayari imefungua ofa ya kumuuza Alexandre Lacazette, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja, huku Granit Xhaka na Lucas Torreira wote wanatarajiwa kuuzwa.

# Benitez apanga kumuuza Rodriguez

**LIVERPOOL, England**

KOCHA mpya wa Everton, Rafael Benitez amedokeza kuna uwezekano mkubwa wa kumuuza mchezaji wake nyota, James Rodriguez kipindi hiki cha majira ya joto.

Hiyo itakuwa ni mwaka mmoja tu tangu mchezaji huyo wa kimataifa wa Colombia alipojiunga na klabu hiyo.

Benitez, ambaye amsaini mkataba wa miaka mitatu kuwanoa Toffees hao mapema mwezi huu, alibainisha kwamba, hataogopa kuuza 'wachezaji wenye mishahara mikubwa' kwani ataweza kutumia fedha hizo kununulia wachezaji wapya.

Rodriguez alionyesha kiwango cha kuvutia katika msimu wake wa kwanza pale Toffees baada ya kujiunga akitokea kwa miamba wa Hispania, Real Madrid, lakini majeruhi ya mara kwa mara yakamfanya kuwa na wakati mgumu wa kupata namba.

Nyota huyo wa kimataifa wa Colombia alianza katika mechi 23 za Ligi Kuu ya England akifunga mabao sita na kwa sasa ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi pale Everton.

Katika mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari tangu ajiunge na klabu hiyo, Benitez, ambaye aliwahi kuwanoa wapinzani wa Everton hapo Merseyside, Liverpool, alidokeza majaliwa ya Rodriguez ingawa hakuwa wazi sana.

"Kila mmoja anajua kwamba klabu hii imetumia fedha nyingi kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita," alisema.

"Kama una wachezaji wenye mishahara mikubwa ambao hawachezi mara kwa mara hivyo suluhisho ni kuwauza ili fedha hizo zitakusaidia kununua wachezaji wapya.

"Hivyo tutajaribu kuliangalia hivyo haraka inavyowezekano ili kuweza kuwa na wachezaji imara kwa kikosi chetu."



## HABARI MICHEZO

# Robben atundika daluga

**AMSTERDAM, Uholanzi**

ARJEN Robben amestaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 37 ambapo kwa mara ya mwisho aliichezea klabu ya Groningen ya nchini Uholanzi katika msimu wa 2020-21.

Robben ameshinda mataji nane ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, mataji matano ya DFB Pokal na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya akicheza pale Bayern Munich.


Robben amefunga mabao 37 na kutoa pasi za mwisho 34 katika mechi 96 katika timu ya Taifa ya Uholanzi.

Majeruhi ya mara kwa mara yamemlazimu nyota huyo wa zamani wa Chelsea kutundika daluga zake.

Robben pia alishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya England akicheza pale Chelsea, mataji mawili ya Ligi, na FA,

Pia amecheza katika klabu za PSV Eindhoven, Real Madrid na Bayern Munich.

Aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Nimeamua kumaliza kipindi changu cha uchezaji soka, yalikuwa ni maamuzi magumu. Napenda kumshukuru kila mmoja kwa kunipa sapoti."




# Saka alia na mitandao ya kijamii kwa ubaguzi

**LONDON, England**

NYOTA wa Timu ya Taifa ya England, Bukayo Saka, amesema kampuni maarufu ya mitandao ya kijamii haijafanya juhudi ya kutosha kuzuia unyanyasaji wa kibaguzi, baada ya yeye kukumbwa na kadhia hiyo.

Saka alikumbwa na wakati mgumu wa kubaguliwa kwenye mitandao ya kijamii baada ya kukosa penalti katika fainali ya Euro 2020 dhidi ya Italia.

Wachezaji waliofanyiwa mabadiliko Marcus Rashford, Jadon Sancho na Saka wote walikosa mikwaju ya penalti ya England ilipofungwa 3-2 na Italia.

Saka ambaye alitoa machozi baada ya fainali hiyo ameomba radhi kwa mashabiki wakati England ikiendeleza ukame wa mataji wa miaka 55.

Saka mwenye umri wa miaka 19 kupitia akaunti yake ya Twitter amewashukuru waliomtumia ujumbe wa kumuunga mkono na kupiga kampeni dhidi ya ubaguzi kwa niaba yake akisema: "Siku zote upendo hushinda."

"Lakini nimeapa kuwa nitakuwa imara dhidi ya ujumbe wa chuki utakaotumwa kwangu kwa njia ya mtandao.

"Kwa mitandao ya kijamii ya Instagram, Twitter na Facebook, sitaki mtoto au mtu mzima yeyote apokee ujumbe wa chuki na kuumiza ambao mimi, Marcus na Jadon tumepokea," alisema Saka.




# Madrid kupunguza kiwango cha mishahara

**MADRID, Hispania**

KIWANGO cha fedha za mishahara ya wachezaji wa klabu ya Real Madrid kinatarajia kupungua kwa karibu pauni milioni 150 msimu huu, kwa mujibu wa The Athletic.

Hatua hiyo itasababisha hatima ya wachezaji wenye mishahara mikubwa kama, Raphael Varane, Gareth Bale na Eden Hazard kuwa katika mashaka.

Wakati wapinzani wao wakuu kwenye soka la Hispania, Barcelona wakiwa katika hali mbaya zaidi kiuchumi huku bado hawajamsajili Lionel Messi kutokana na athari za mlipuko wa virusi vya corona, Real Madrid imeshuhudia mapato yakishuka kwa kiasi kikubwa.

The Athletic imesema msimu uliopita kiwango cha fedha za mshahara wa wachezaji klabu hiyo kwa sheria za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kilikuwa pauni milioni 403.

Laini sasa kinatarajiwa kushuka hadi pauni milioni 255 kwa msimu mpya unaotarajia kuanza mwezi ujao.

Matokea yake inasemakana lengo kuu la Real Madrid msimu huu ni kupunguza kikosi cha kwanza chenye wachezaji 35 kwa sasa.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HALAAND AOTA MBAWA CHELSEA

**DORTMUND, Ujerumani**

●●● Dau lao la pauni mil. 150 na straika mmoja lakataliwa Dortmund wakitaka...

BORUSSIA Dortmund imeikataa ofa ya Chelsea ya kutaka kumsajili straika wake, Erling Haaland, kwa mujibu wa Sky Ujerumani.

Chelsea walitoa ofa rasmi ya pauni milioni 150 kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway, ambapo mmiliki wake, Roman Abramovich anatajwa kuwa shabiki wake mkubwa.

Inaeleweka kwamba, Chelsea ilikuwa tayari kuwapa Dortmund kati ya Tammy Abraham au Callum Hudson-Odoi katika dili hilo la kumnunua Haaland, lakini miamba hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wamepanga kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20.

**Blues hao walipanga kutaka kumsajili mshambuliaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto baada ya kutokuwa na safu imara ya ufungaji msimu uliopita.**

Licha ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel hakikuwa na nafasi kubwa ya kufunga mabao kwa kuwa Timo Werner na Abraham kila mmoja alifunga mabao 12 na kuwafanya wafungaji bora wa klabu hiyo.

Hata hivyo, Sky Sports News imetonywa kwamba, winga Hudson-Odoi "hatakuwa sehemu ya dili linalohusisha uhamisho wa Haaland."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 anatajwa kuwa na "mahusiano ya kuvutia" na kocha mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel na anaonekana kuwa na majaliwa ya muda mrefu klabuni hapo, hatakama atakuwa na wakati mgumu wa kugombania namba kwenye kikosi cha kwanza kwa misimu inayokuja.

Haaland anaonekana kuwa ndio chaguo la kwanza kwa Chelsea na majadiliano yalikuwa yakifanyika kwa ajili ya kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto, lakini sasa dili hilo limeyeyuka.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya Sky Sports News dili hili sasa linatajwa kama "lisililowezekana tena."

Kushindikana kwa dili hilo pia kunamhusisha wakala wa Haaland, Mino Raiola ambaye anataka kupata kiasi cha euro milioni 40 katika usajili huo.

Pia baba wa Haaland naye anataka kupatiwa kiasi cha euro milioni 10 katika usajili wa mwanawe huyo.

## KWA UFUPI

**SPURS WAMTAKA PELLEGRINI**
TOTTENHAM Hotspur, wanaweza kumsajili kiungo wa kati wa AS Roma, Lorenzo Pellegrini mwenye umri wa miaka 25, lakini watatakiwa kutoa kitita cha pauni milioni 26 kumnasa Muitaliano huyo.(***Athletic*** )

**ABRAHAM AWANIWA ARSENAL**
ARSENAL wanamtaka mshambuliaji wa Chelsea, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23 ambaye awali alikuwa anawaniwa na Tottenham na Inter Milan. (***Mail***)

**KANE, LUKAKU NA CHELSEA**
CHELSEA wanalenga kusajili washambuliaji wawili, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 kutoka Tottenham Hotspur na Romelu Lukaku wa Inter na Ubelgiji mwenye umri wa miaka 19. (***Telegraph***)

**ANCELOTTI AMWANIA SALAH**
KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amewataka viongozi wa klabu hiyo kumsajili mshambuliaji Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 29 kutoka Liverpool. (***Fichajes***)

**INGS ATAKIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili mshambuliaji, Danny Ings, lakini wanakabiliwa na ugumu kwasababu Southampton wanasita kufanya biashara na klabu hiyo ya kaskazini mwa London. (***Standard***)

**LINGARD HUYO ATLETICO**
MABINGWA wa Ligi Kuu ya Hispania, Atletico Madrid, wanahusishwa na taarifa za kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard, ambaye anatolewa macho na West Ham. (***90min***)

**VLAHOVIC KUPEWA MKATABA**
FIORENTINA wanapanga kumpa mkataba mpya nyota wao, Dusan Vlahovic raia wa Serbia ambaye anamezewa mate na Liverpool na Tottenham. (***Calciomercato***)

**VARANE ANUKIA MAN UNITED**
REAL Madrid wameridhia kuwa mchezaji wa nafasi ya ulinzi, Raphael Varane hatasaini mkataba mpya na wanasubiri ofa ya Manchester United. (***Goal***)

**BRENTFORD WAMTAKA AJER**
KLABU ya Brentford inajiandaa kuweka mezani ofa ya pauni milioni 13.5 kwa ajili ya mlinzi wa Celtic, Kristoffer Ajer mwenye umri wa miaka 23. (***Sun***)

**PALMIERI AGOMBEWA**
MLINZI wa Chelsea, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26, anatakiwa na Inter Milan na AS Roma. (***Calciomercato***)

**WILLOCK KUBAKI NEWCASTLE**
NEWCASTLE United inawania kumsajili nyota wa Arsenal, Joe Willock mwenye umri wa miaka 21 kwa mkataba wa kudumu, baada ya kucheza hapo St James' Park kwa mkopo msimu uliopita. (***Chronicle***)

**MILAN WAKATA OFA YA PSG**
KLABU ya AC Milan wamekataa ofa ya pauni milioni 34 kutoka Paris St-Germain kwa ajili ya kumuachia kiungo wao wa kati, Theo Hernandez mwenye miaka 23. (***Tuttosport***)

HABARI MICHEZO

# METACHA KUIONGOZA U-23 MICHUANO CECAFA ETHIOPIA

**Na Saada Akida**

GOLIKIPA wa Yanga, Metacha Mnacha ametajwa katika kikosi cha wachezaji 20 watakaokwenda kupeperusha bendera ya Tanzania Bara katika mashindano ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 23 (U-23), ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yatakayofanyika jijini Addis Ababa nchini Ethiopia.

Michuano hiyo inatarajiwa kufanyika kuanzia kesho Jumapili hadi Julai 31, mwaka huu.

Hata hivyo, Metacha ameitwa katika kikosi hicho huku akiwa amesimamishwa na klabu yake kutokana na utovu wa nidhamu, lakini pia akitumikia adhabu ya kusimamishwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya kuonyesha ishara ya matusi katika mechi dhidi ya Ligi Kuu dhidi ya Ruvu Shooting.

Katika mashindano hayo, Tanzania Bara imepangwa kundi moja na Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na itashuka kuanza kampeni ya kuwania taji hilo Julai 22, mwaka huu dhidi ya waalikwa Wakongomani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kim Poulsen alisema hajaita wachezaji kutoka katika timu za Simba na Yanga kwa sababu wako katika majukumu ya maandalizi ya mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Poulsen alisema ameamua kutoa nafasi kwa wachezaji wengine ili kuonyesha vipaji vyao na kupata nafasi ya kuitumikia nchi yao kwa wakati huu.

"Tumeshindwa kuwaita wachezaji wa timu hizo, akiwamo Feisal Salum 'Fei Toto' na wengine ambao wako katika majukumu ya klabu zao, ila tunaenda kupambana na kuhakikisha tunafanya vizuri katika michuano hiyo," alisema Poulsen.

Alikitaja kikosi kamili cha timu hiyo kinaundwa na Metacha, Daniel Mgore, Abdulmajid Magalo (Biashara United), Wilbol Maseke, Pascal Msindo (Azam FC), Israel Mwenda (KMC FC), Nickson Kibabage (Youssoufia FC - Morocco), Lusajo Mwaikenda (KMC FC), Oscar Masai (Ihefu), Lucas Kikoti (Namungo) na Joseph Mkele wa Mtibwa Sugar.

Wachezaji wengine ni Rajab Athumani, Meshack Abraham (Gwambina FC), Eric Mwijage (Kagera Sugar), Andrew Simchimba (Ihefu), Abdul Suleiman (Coastal Union), Pascal Msindo (Azam FC), Abdulrahman Hamza (Mbeya City), Abdulmajid Mangalo (Biashara United) na Yusuph Mhilu wa Kagera Sugar.

Tanzania Bara itashuka tena dimbani Julai 25, mwaka huu kucheza dhidi ya Uganda na timu nne zitakazokuwa zimefanya vizuri zitasonga mbele katika mashindano hayo.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu kutoka sehemu mbalimbali Dar es Salaam wakifanya mazoezi ili kujiimarisha katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Vita ya kushuka daraja mbichi

**Na Adam Fungamwango**

MATOKEO ya mechi za raundi ya 33 ya Ligi Kuu, yameifanya vita ya timu zinazopigana kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara, na zile zinazojipapatua kutoingia kwenye mtego wa kucheza mechi za mtoano kuwa bado ni kubwa, sasa hatima itapatikana kwenye mechi za mwisho wa Ligi Kuu, Jumapili.

Ni timu tano za Simba, Yanga, Azam, Biashara United na KMC, ndizo zipo salama, lakini kuanzia nafasi ya sita inayoshikiliwa na Tanzania Prisons, hadi nafasi ya 17, inayoshikiliwa na Gwambina FC, bado hazina uhakika wa kubakia katika Ligi Kuu au kuepuka kucheza motano maarufu 'play off'.

Ushindi wa mabao 5-0 iliyoupata Coastal Union dhidi ya Mwadui ambayo tayari imeshuka daraja, umeifanya timu hiyo kutoka kwenye nafasi ya 17 na kupaa hadi ya 14 ikiwa na pointi 37, ikisubiri majaliwa kwenye mechi ya mwisho dhidi ya Kagera Sugar.

Suluhu iliyoipata Mtibwa Sugar dhidi ya Dodoma Jiji, umeifanya timu hiyo kutoka kwenye nafasi ya 11 na kushuka nafasi mbili chini hadi ya 13 kwa pointi 39, ikiwa kwenye hatari zaidi ya kushuka daraja msimu huu. Mechi yake ya mwisho dhidi ya JKT Tanzania ndiyo itaamua, huku timu zote mbili hizo zikipumulia mashine.

Mbeya City iliitungua Gwambia bao 1-0, lakini pamoja na ushindi huo imeruka kwenye nafasi moja tu kutoka ya 13 na kwenda hadi ya 12, ikimiliki pointi 39 huku kipigo cha mabao 2-0 ilichopata Ihefu FC kutoka kwa Yanga kimeifanya kuteremka kutoka nafasi ya 15, hadi ya 16, ikibaki na pointi zake 35 tu.

Kagera Sugar ilishinda bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania, na kuifanya kutoka nafasi ya 12, hadi ya 11 lakini JKT Tanzania iliyofungwa mabao 5-2 na KMC imeendelea kudidimia kutoka nafasi ya 14 hadi ya 15, huku Ruvu Shooting ikishinda mabao 2-1 dhidi ya Namungo FC ikiwa mkakati ya kuepuka kwenda kucheza 'play off', hivyo kufikisha pointi 41, ikiwa kwenye nafasi ya 10.

## Namungo yazionya timu kimataifa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo FC imezitahadharisha timu ngeni zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa kujiandaa vyema hasa katika suala la fedha kwa sababu michuano hiyo ni migumu na inatumia gharama kubwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Namungo, Omari Kaaya aliliambia gazeti hili walichojifunza kwenye michuano ya kimataifa ni kuwa haiwezekani kufanya vyema kama klabu haina fedha au kutegemea 'kupitisha bakuli', hivyo klabu yoyote ambayo haijawahi kucheza michuano hiyo au hata ambazo zimecheza miaka kadhaa nyuma zijiweke imara.

"Kwanza timu ikishiriki michuano hiyo ijue kuna gharama kubwa sana hasa ikienda kucheza ugenini. Sisi tulitumia kiasi cha Sh. milioni 60 hadi 70 kwa safari kwenda kucheza ugenini na kiasi cha Sh. milioni 10 kama tunacheza hapa nchini kwa ajili ya kuwalipa waamuzi, hoteli, usafiri na gharama nyingine," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Alisema kwenye kipindi hiki cha maambukizo ya ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, gharama pia zimeongezeka pamoja na changamoto nyingine, kama vile kuwapima wachezaji hapa nchini na pia hata nchi wanayokwenda wanapima tena, huku wachezaji wote wakitakiwa kulipiwa gharama za upimaji.

## Vipaji vyatawala Shule ya Joyland

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wa Shule ya Kimataifa ya Joyland ya Toanganoma Kigamboni jijini Dar es Salaam, wametia fora katika bonanza ambapo wameonyesha vipaji vya aina mbalimbali.

Katika bonanza hilo, wanafunzi hao walionyesha umahiri kwenye kuigiza michezo mbalimbali ikiwamo mashindano ya kula kwa haraka.

Miongoni mwa vitu vilivyotia fora kwenye bonanza hilo ni mbio fupi na ndefu, kukimbia na magunia, kuruka viunzi na namna walivyomudu kuwasilisha sanaa hiyo kwa ubunifu mkubwa.

Mwalimu wa michezo wa shule hiyo, Jonathan Mbogoma, alisema waliandaa bonanza hilo kwa ajili ya kuendeleza vipaji vya wanafunzi hao kwenye fani mbalimbali na kwamba hufanyika mara tatu kila mwaka.

Alisema mbali na masomo ya darasani, shule imeona umuhimu wa kuwakutanisha wanafunzi hao kwenye bonanza ili waonyeshe vipaji vilivyonavyo kwenye muziki wa bongo fleva na maonyesho ya mitindo ya mavazi.

"Mbali na masomo ya darasani tumeona kuna umuhimu wa kubaini vipaji vya wanafunzi na kuvikuza mtoto lazima alelewe katika nyanja mbalimbali kwasababu mwisho wa siku anaweza kuishi kutegemea kipaji chake," alisema.

# Michezo

Jumamosi Julai 17, 2021

Nipashe



HAALAND AOTA MBAWA CHELSEA HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Simba, Medie Kagere (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Azam FC, Daniel Amoah katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam juzi usiku. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. PICHA: JUMANNE JUMA

## SIMBA KUPOKEA KIKOMBE KIBABE

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes amesema wachezaji wake wamepambana na wameahidi kutoa burudani katika mechi ijayo dhidi ya Namungo FC ambapo watakabidhiwa kombe lao ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Gomes alisema kulikuwa na mabadiliko ya baadhi ya wachezaji katika mechi mbili na lengo ni kuwapumzisha wachezaji waliotumika sana kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaochezwa dhidi ya watani zao, Yanga. Gomes alisema nyota waliopewa nafasi ya kucheza wamefanya vizuri katika mechi hizo mbili na anatarajia kuwatumia pia kwenye mchezo wa mwisho dhidi ya Namungo FC ambao ni siku muhimu kwao kutokana na kukabidhiwa ubingwa.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri katika mechi zetu zote, hatujapata matokeo mazuri sana ambayo tulitarajia, kupoteza nafasi nyingi za mabao dhidi ya Azam FC , niliowapa nafasi wamepambana na kupata matokeo mazuri, tunarejea katika mazoezi kwa ajili ya mechi ijayo."

"Kuhusu washambuliaji watatu kuwatumia katika mechi ya leo (juzi), ilikuwa hatari kwangu kwa sababu anaweza kupata jeraha na kuharibu mipango yetu kuelekea mechi ya FA," alisema Gomes.

Aliongeza ana imani katika mechi ijayo dhidi ya Namungo FC watapata matokeo mazuri ili kuendelea kunogesha ubingwa waliouchukua kwa msimu wa nne mfululizo.

Gomes ameibuka kocha bora wa mwezi Juni, baada ya kukiongoza kikosi hicho kushinda kwenye michezo mitatu ambayo walicheza dhidi ya Ruvu Shooting, Simba, Polisi Tanzania dhidi ya Mbeya City huku John Bocco akichaguliwa kuwa mchezaji

# *Uchaguzi Mkuu TFF pale pale*

## ●●● Mahakama yaruhusu mchakato kuendelea baada ya ...

**Na Kulwa Mzee**

MAOMBI ya kuzuia kwa muda uchaguzi wa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) yametupwa baada ya Mahakama Kuu kuona hayana msingi. Uchaguzi Mkuu wa unatarajiwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu jijini Tanga.

Uamuzi huo ulitolewa jana na mahakama hiyo mbele ya Jaji Edwin Kakolaki baada ya kusikiliza hoja zilizobishaniwa na pande mbili. Mlalamikaji aliyetaka uchaguzi usimamishwe katika shauri hilo ni Ally Salehe na mlalamikiwa ni Bodi ya Wadhamini ya TFF, TFF na Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi ambao waliomba maombi yatupwe na uchaguzi uendelee.

Katika uamuzi wake, Jaji Kakolaki, alisema kuwa baada ya kupitia hoja zote, mahakama imeona mlalamikaji ameshindwa kuonyesha kuna madai ya msingi katika kesi na ameshindwa kuonyesha madhara au hasara anayoweza kupata endapo mahakama haitatoa amri aliyoiomba.

Jaji Kakolaki alisema mlalamikaji alitakiwa kuonyesha kuna haki katika kesi ya msingi inayohitaji kuilinda lakini hakufanya hivyo.

"Hii si kesi sahihi ya kuweza kutoa amri ya zuio, hivyo mahakama inayatupilia mbali maombi hayo na kila upande utajighara-mia," alisema Jaji Kakolaki.

**Mahakama haikukubali ana na hoja za Wakili wa Mlalamikaji, Jeremiah Mtobesya, aliyedai mteja wake aliondolewa katika mchakato kwenye hatua ya mahojiano wakati alitakiwa kuhojiwa halafu taarifa zake kuwekwa katika ubao wa matangazo.**

Alidai utaratibu umekiukwa na madhara yake hayawezi kufidiwa, mlalamikaji atapata hasara, hivyo akaiomba mahakama kuzuia mchakato wa uchaguzi.

Alidai endapo amri hiyo haitatolewa mlalamikaji atapata hasara kwani ndiye anayeweza kupoteza zaidi kuliko TFF.

Mahakama ilikubaliana na hoja za Wakili wa Walalamikiwa, Alex Muchunguzi, aliyedai kwamba katika kiapo cha mlalamikaji, hakuna hoja za msingi za kuifanya mahakama ifikie uamuzi wa kutoa zuio la muda la uchaguzi hadi kesi ya msingi namba 98 itakaposikilizwa. Alidai hakuna mahali popote katika hati ya kiapo ambapo mlalamikaji aliandika malalamiko ya kukiukwa kwa utaratibu, kutokuwapo kwa taarifa zake katika ubao wa matangazo.

Mahakama ilikubali hoja kwamba kutolewa kwa zuio kutamwathiri zaidi mlalamikiwa namba mbili, yaani TFF, ambaye anaweza kufungiwa na Shirikisho la Kimataifa la Mpira wa Miguu (FIFA).

Miongoni mwa masuala anayolalamikia mlalamikaji, ni upungufu uliomo katika Katiba ya TFF ikiwamo suala la ubaguzi katika katiba hiyo kuhusiana na uchaguzi.

Anasema kuwa kwa mujibu wa Katiba, mgombea urais anatakiwa kuidhinishwa na vyama vya mikoa au shirikishi zaidi ya vitano wakati Zanzibar hakuna wajumbe wa kamati hiyo.

Rais wa TFF, Wallace Karia ambaye anatetea nafasi hiyo, anasubiri kuthibitishwa na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa shirikisho hilo kwa sababu hana mpinzani, lakini kinyang'anyiro kikibakia kwenye kanda ambapo zimepungua kutoka 13 hadi sita.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002